
SUPA JACKPOT
TZS. 1,114,965,687
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MBOWE** asema hawatashiriki uchaguzi bila Katiba mpya


BUFE
Nipashe
HIFADHI YA KATAVI
Samia na Royal Tour, wageuka nyenzo ya ushindi soko watalii
• Rasmi, aliyoyatamka kwenye uzinduzi...
Darasa mazingira na biashara ililyoyinua wanawake wafugaji kijasiriamali, kuimiliki

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Mei 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581315

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Utitiri wa minara wamshtua Rais Samia

UKURASA 2

## Haya ndiyo mambo yaliyokera wafanyabiashara wa Kariakoo

**HATIMAYE** biashara zarejea rasmi ...

*Endelea ukurasa 2 & 4*




Maduka yakiwa yamefunguliwa katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana, baada ya wafanyabiashara kusitisha mgomo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**




Rais Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo wakati mtoto Georgina Magesa (8) akiwa ameketi kwenye kiti chake, baada ya kukutana naye katika uzinduzi wa minara ya kurusha matangazo ya Televisheni Ardhini (DTT) ya Azam Media, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rushwa ngono sasa yatikisa mikopo umiza

UKURASA 3

**MICHEZO** RAIS SAMIA AIPA NDEGE YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mkaguzi wa Polisi wa Kituo cha Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Godson Mongo, akishiriki kuchimba msingi, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi, Lwiza Mlelwa wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utitiri minara wamshtua Rais Samia

**Na Mauld Mmbaga**

UTITIRI wa minara ya mawasiliano nchini, umemshtua Rais Samia Suluhu Hassan huku akiitaka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutafuta teknolojia ya kuchanganya huduma kwenye mnara au chombo kimoja.

Pia amesema serikali iko katika hatua za mwisho za kuanzisha kituo cha setelaiti ili kurahisisha mawasiliano na kusambaza maudhui ya Kitanzania.

Rais Samia aliyasema hayo jana Dar es Salaam, wakati akizindua mradi wa minara ya kurusha matangazo ya televisheni ardhini (DTT) wa kampuni ya Azam Media katika mikoa 21 nchini.

Samia aliipongeza Azam kwa kuendelea kufanya uwekezaji wa mitambo ya kisasa Watanzania kupata matangazo yenye ubora popote walipo.

Alisema mwezi huu alizindua minara 758 iyakayojengwa na kampuni ya simu na mingine zaidi ya 300 inatakayoongeza uwezo.

Jana, kampuni ya Azam ilizindua mradi wa minara 21 ambayo imejengwa katika mikoa mbalimbali nchini ambao uligharimu takribani Sh. bilioni 50.

"Nilimuuliza Waziri (wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye) hakuna teknolojia ya kwenda kuchanganya yote (minara) yakaingia pahali pamoja kwa sababu nchi yote itajaa minara hii. Kila unapokwenda minara, ukiuliza huu wa Azam, huu wa Tigo, huu wa Voda. Nchi yote itajaa minara, kwa hiyo nadhani tufanye kazi ya kutafuta teknolojia ya kuchanganya," aliagiza.

Aliongeza kuwa katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo ya kwanza kuhamia katika teknolojia ya kidigitali, huku akisifia minara ambayo aliizindua jana kwamba italifanya taifa kuwa la kwanza ambayo itawapatia huduma kwenye simu janja bila kuwa na laini ya simu.

Pia alibainisha kuwa serikali iko katika hatua za mwisho za kuja na mpango wa kutumia setelaiti katika kurusha matangazo na kwamba wamejipanga vizuri na tayari wameshaanza mazungumzo huku akiwahakikishia Watanzania kuwa mpango huo utakamilika.

"Nilikuwa naongea na Tido Mhando mimi nina ki-studio kidogo tu lakini kinanishinda, kinadhorota kwa hiyo hebu vuka maji kanisaidie, sasa uwekezaji kama huu ukiona kwa mwenzio lazima u-salute na uheshimu, hongereni sana," alipongeza Rais Samia.

Alisema hayo ni mageuzi makubwa na ni jambo la kujivunia kama taifa, akieleza kuwa wanapoweka nguvu kubwa ya pamoja kwa sekta binafsi na serikali na kufikia hatua hiyo ni jambo la kujivunia.

**VYOMBO BINAFSI**

Rais Samia alisema amefarijika kuona sasa kumekuwa na mwelekeo mzuri baada ya utekelezaji wa maagizo aliyompa waziri wa habari na timu yake wakati akiwaapisha.

Alisema amefurahishwa kusikia kwamba wizara imekutana mara kadhaa na wadau ili kupokea maoni yao na kujadiliana kuhusu marekebisho ya kanuni na sheria na kwamba ni matumaini yake kuwa sheria itakapotoka haitakuwa tena na malalamiko.

"Uhusiano baina ya vyombo vya serikali na binafsi umeimarika sana, najua kwenye kuzungumza hakukosekani suluhu, mnapozungumza mkajua shida ni nini na matatizo yako wapi ndipo mnapopata mwanya au fursa ya kurekebisha yaliyopo na tukaenda," alisema.

"Sheria na kanuni peke yake na kusimama kwenye hizo hakutatui matatizo bali huongeza matatizo, nikupongeze waziri na timu yako na vyombo binafsi kwamba sasa mumeamua kukaa pamoja kuzungumza na kutatua matatizo yaliyopo na sasa tunakwenda vizuri, kelele zimepungua," alisisitiza.

**UHURU WA HABARI**

Mbali na kwamba vyombo vya habari sasa vina uhuru na kuandika wanayoyataka, alisisitiza kuwa ni muhimu kufuata mila na desturi za nchi, ikiwamo kuheshimiana kwamba vyombo viheshimu navyo viheshimiwe.

"Hilo ni la kwanza lakini la pili, uhuru maana yake ni kujiweza, kujitegemea na kujiendesha ndipo utakuwa huru. Lakini unataka kuwa huru kusema, kisha unarudi serikalini tubebe tusaidie ili tuweze kusema.

Hapana uhuru hapo, sasa kama vyombo vinataka kuwa huru vijiweze na kujiendesha," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
19.05.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 20-05-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Bulyanhuru** kupitia Dodoma, gari hizo zina namba za usajili: **T 868 DXS / T 837 CHK, T 776 EAP / T 128 ECL**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 22.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.30** |
| **Kimo** | - | **mita 5.10** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Bulyanhuru kupitia Dodoma,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

# Haya ndiyo mambo yaliyokera wafanyabiashara wa Kariakoo

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA katika eneo la Kariakoo wameeleza vikwazo vinavyowasumbua kiasi cha kuzorotesha shughuli zao, hivyo kulazimika kutumia njia za mkato kuendelea na biashara.

Aidha, wako waliofunguliwa kesi za uhujumu uchumi na wanazungushwa kila siku na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), huku wengine wakipoteza maisha, kupata magonjwa yasiyoambukiza, msongo wa mawazo, kufuatwa hadi nyumbani na baadhi kufilisika, mbali na madhila hayo, wengine waliamua kufunga biashara kukubali yaishe.

Yote hayo yalibainika juzi baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwapa nafasi wafanyabiashara waliokuwa wamekusanyika viwaja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam kueleza kero zinazowakabili baada ya mgomo wa siku mbili mfululizo.

Wako walioeleza wanavyokabiliwa na kesi na katika hali isiyo ya kawaida, siku hiyo walipofika mahakamani, waliambiwa zimeondolewa kwa ajili ya mazungumzo na TRA namna watakavyolipa wanachodaiwa huku kukiwa na kubambikiwa kodi na madai hewa.

**KESI UHUJUMU**

Akizungumza katika mkutano huo, mfanyabiashara wa vitenge, Salome Keiovu, maarufu kama Mama Bonge, alisema tangu mwaka 2021, hawaingizi vitenge kupitia Bandari ya Dar es Salaam kutokana na ushuru kuwa mara kumi zaidi ya Kenya.

Alisema ushuru wa makontena ya vitenge yanayopakuliwa Bandari ya Dar es Salaam ni Sh. milioni 200 hadi 240, wakati Zambia ni dola 10,000 (takribani Sh. milioni 24) na Kenya ni Sh. milioni 45, hivyo kulazimika kuagiza bidhaa hiyo kutoka nchi jirani.

Keiovu alisema Novemba, mwaka jana, TRA walikamata makontena 10 ya vitenge na baada ya kufanyiwa ukaguzi, akaambiwa ailipie Sh. bilioni 10.3 na aliposhindwa kulipia, Aprili 14, mwaka huu, alipelekewa barua ya kushtakiwa kwa uhujumu uchumi.

Alisema alisita kwenda mahakamani hadi juzi alipoamua kwenda na alipofika aliambiwa kuwa kesi yake imefutwa na jana yake usiku alipigiwa simu na maofisa wa TRA kwamba akachukue mzigo wake.

Kwa sasa, anasema hana kiasi hicho cha pesa kwa kuwa hajafanya biashara kwa miezi minane na aliwaomba TRA alipe Sh. milioni 150 ili wafanye mazungumzo lakini walikataa na kumsisitiza alipe Sh. bilioni 3.4.

**AFUATWA NYUMBANI**

Mfanyabiashara wa vipodozi, ambaye jina lake halikufahamika, alisema maofisa wa TRA wameweka mbele maslahi binafsi kiasi cha kuwafuata nyumbani kutaka rushwa pale wanapowakosa dukani.

**RUSHWA**

Mfanyakazi wa kampuni ya kusafirisha mizigo mkoani Kigoma, Aram Nyenge, alisema maofisa wa TRA Kigoma, wamekuwa wakiwamata na kukagua mizigo ya wateja na kuwataka watoe rushwa kwa madai kuwa mizigo haina thamani ya kodi ya ushuru iliyolipiwa ilhali ilishakaguliwa Dar es Salaam.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakiwaambia washirikiane kudai rushwa kwa wateja kwa kuwapa namba za simu kisha wakishatoa pesa watawagawia posho.

Hali hiyo, alisema ilisababisha wateja wengi kusitisha kununua bidhaa Dar es Salaam na kuhamia Burundi, Uganda na Kenya huku wafanyabiashara wa soko la Kariakoo wakilia biashara ngumu. Kutokana na usumbufu huo alikwenda kutoa taarifa katika ofisi za TRA Dar es Salaam na maofisa hao walitwa na kuelezwa lakini bado tabia hizo zinaendelea.

Mfanyabiashara wa nguo za kike Kariakoo, Irene Mmari, alisema tangu Novemba, mwaka jana, mauzo ya biashara yake yameshuka hadi kufikia Sh.300,000 kwa mwezi kutoka Sh. milioni 5,000,000 kutokana na wateja wake wakubwa ambao ni raia wa Malawi na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo(DRC) kusitisha kununua bidhaa hizo nchini.

Naye Elimringi Goodluck alisema kulipa kodi ya stoo kila mwezi ni mzigo mkubwa kwao kwa kuwa wanalipa pesa ya pango kwa wenye stoo, hivyo wao ndio wanapaswa kilipia kodi hizo.

Alisema cha ajabu ni kuwa TRA waliwaambia kuwa kodi hiyo ni kifungu cha 45 atakayekiuka, atalipa faini ya Sh. milioni tatu hadi 4.5 na kuwa inatengeneza mianya ya rushwa kwa sababu ofisa wa TRA ndiye anayeamua kiasi cha faini ya kumtoza mfanyabiashara aliyekiuka kuilipa.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, akiwasilisha makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rushwa ya ngono yatikisa mikopo umiza

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

MIKOPO kichefuchefu, rusha roho, komandoo, miyeyusho, pasua kichwa na kausha damu, ambayo yote ni maarufu kama mikopo umiza, imewaibua wabunge na kusema imekuwa ikiwaumiza wanawake.

Baadhi ya wabunge wamesema wako baadhi ya wanaume wamekuwa wakitumia mikopo hiyo kama sehemu ya rushwa ya ngono baada ya wahusika kukosa marejesho.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akihitimisha hoja za wabunge waliochangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24, alisema atafika kwenye ofisi hizo ili kujua waliowasajili na kuwapa vibali.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka, akichangia kwa mara ya kwanza baada ya kuugua mwaka mzima na kulazwa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma, alisema mitaani kuna mikopo inayoitwa kichefuchefu, kibangala, rusha roho, komandoo, miyeyusho pasua moyo .

"Hayo yote ni mikopo ambayo kinamama wanahangaika nayo na mingine inawadhalilisha," alisema.

Katika taarifa yake, Mbunge wa Viti Maalum, Felister Njau, alisema anataka kumwongezea mchangiaji kwamba kuna mkopo unaoitwa kausha damu na sasa umesababisha wanawake wengi wameachika kwenye ndoa na kufilisika kwa sababu una riba kubwa na mkopaji analipa kwa siku.

Akiendelea kuchangia, Malembeka aliipokea taarifa hiyo na kusema, hiyo ni pamoja na ile aliyoitaja ambayo inawadhalilisha wanawake.

"Kuna mikopo ambayo kinamama badala ya kwenda kuilipa unakwenda kulipa mwili badala ya fedha. Kuna wanaume wamekaa tayari wanaitwa 'mzee wa vikoba', yaani mama akakope yeye kazi yake kulipa tu lakini analipa mwili. Hii inatudhalilisha wanawake. Waziri pita kwenye hivyo vikoba pitia angalia wanakwendaje, tutakwisha magonjwa mengi," alisema.

Waziri Gwajima alisema utitiri wa mikopo umelalamikiwa na kwamba anashukuru Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi limeanza.

"Wanawake wote wanaolia machozi sasa yasiyoeleweka wanakwenda kupona. Wanakwenda kuziona fursa nyingine tofauti kabisa za mikopo nafuu kupitia majukwaa haya.

"Sasa hawa wanaojiita mikopo ya makomandoo sijui mikopo pasua kichwa, damu na nini, mimi niwaombe huko mliko majukwaa yameanza na mtaniona mpaka kwenye ofisi zenu mniambie mlisajiliwa na nani? Mlipewa kibali na nani katika kuwapatia wanawake mikopo ambayo pengine haikidhi hadhi ya utoaji mikopo.

"Waende wakajisajili kwenye taratibu sahihi, wapewe miongozo ya utoaji mikopo. Kwa hiyo ukombozi wa wanawake Mheshimiwa Spika umefika kupitia haya majukwaa,"alisema.

**TAARIFA YA USHOGA**

Waziri Gwajima alisema hivi karibuni wizara iliapata taarifa za wanaharakati ambao walikuwa wakishirikiana na Waziri mstaafu, Dk. Harrison Mwakyembe, kusema kwamba kuna hiyo hali huko kwenye jamii baadhi ya mashirika yanahusishwa kuchochea vitendo hivyo.

"Wizara imechukua hatua ya kuyaita yale mashirika yote yaliyotuhumiwa kule kupitia sheria ya msajili wa haya mashirika, wakaambiwa watoe maelezo. Baadhi yao wameshawasilisha maelezo na wengine wanayawasilisha.

"Kwa sababu suala hili ni la kisheria tukasubiri hayo maelezo yakamilike ili yaweze kuchanganuliwa na bodi ya usajili ili yawasilishwe kwa mujibu wa sheria, kama kutakuwa na mtu ataona ameonewa sheria inasema rufani iende kwa waziri, mimi nitapokea, kwa sasa mchakato unaendelea uwasilishaji hayo maelezo kujibu zile tuhuma walizohusishwa nazo," alisema.

**NGO ZILIZOFUTWA**

Alisema hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeyafuta mashirika 4,898 kati ya 14,059 yaliyokuwa na usajili baada ya kubainika kutozingatia sheria.

Alisema katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kukusanya Sh. bilioni 8.5 kutoka kwenye ada za wanafunzi, uuzaji wa Mitaala ya kufundishia fani za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na malipo ya hosteli katika vyuo sita vya Maendeleo ya Jamii na viwili vya Maendeleo ya Jamii Ufundi lakini kadi kufikia Aprili, ikakusanya Sh. bilioni 3.025 sawa na asilimia 35.59.

Alisema kushuka kwa makusanyo ya mapato kunatokana na wanafunzi wengi kutoripoti kama ilivyokadiriwa na vyuo pamoja na kufuta usajili wa mashirika hayo kumeathiri makusanyo.

# Mbowe: Hatuendi kwenye uchaguzi mkuu 2025 bila Katiba mpya

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema chama hicho hakiko tayari kwenda kwenye uchaguzi mkuu bila Katiba mpya, sheria mpya ya uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi.

Pia amesema uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulivurugwa kwa kutumia udhaifu kwenye maeneo hayo, hivyo kwenda katika uchaguzi mwingine kwa mazingira yale yale, watakuwa wanafanya makosa makubwa.

Mbowe alisema hayo jana akiwa kwenye Kata ya Gwarama, Buyungu mkoani Kigoma ambako chama hicho kinaendelea na mikutano ya hadhara ya kudai katiba mpya iliyopewa jina la +255 Katiba Mpya.

Alisema chama hicho kilipita katika wakati mgumu kwa kipindi cha miaka saba iliyopita kwa misimamo yao ya kukataa kununuliwa huku baadhi yao wakiteswa, kubambikiwa kesi na wengine kupoteza maisha.

"Miaka saba yote tulipitia wakati mgumu sana, kwenye bonde la uvuli wa mauti. Tulikataa kununuliwa lakini cha mtemakuni tulikiona. Mahakama zilituhusu, wabunge na madiwani walinunuliwa na watu waliteswa na wengine Mungu hakuwapa bahati ya kuvuka. Demokrasia na uchaguzi vilivurugwa,"alisema Mbowe.

"Kwa hiyo sasa hivi si wakati wa kulalamika bali wa kujipanga ili kwenda kupata ushindi tuliouzoea siku zote. Tunataka kuandaa madiwani wajao, tunataka kujipanga kwa ubunge na hatimaye kwa urais na kuirejesha kwenye chama cha CHADEMA ndiyo maana tumeona kuzunguka nchi nzima kujiandaa mapema kwa mabadiliko yatakayokuja baada ya kufanywa kwa mabadiliko ya sheria ya uchaguzi, Katiba na Tume Huru.

"Yale yaliyotokea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yalisababishwa na Katiba mbaya tuliyo nayo leo. Kila kitu kilichofanyika kilikuwa kwa kutumia vibaya sheria zetu za uchaguzi. Tutakuwa tunafanya makosa makubwa kama tutarudi kwenye uchaguzi mkuu kwa sheria hizi, kwa tume hii ya uchaguzi na kwa Katiba hii.

"Sisi kama chama kikuu cha upinzani, agenda yetu kubwa ni kuipata Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi ili tuwe na chaguzi ambazo hazipendelei chama chochote wala ambazo hazisimamiwi na upande mmoja, Tunataka kuanzia uchaguzi wa wenyeviti wa serikali za mitaa, madiwani, ubunge na rais usimamiwe na tume huru ya uchaguzi itakayoundwa kwa kutumia sheria mpya ya uchaguzi," alisisitiza.


## KUPOTEA KWA VYETI



**ERICK REUBEN SHAYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0101-0142** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AZANIA SEKONDARI** mwaka 2000. Cheti cha Advanced Diploma in Accountancy kilichotolewa na **INSTITUTE OF ACCOUNTACY ARUSHA** mwaka 2007. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/URA/RB/169466/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**SHAURI LA MADAI No. 144/2023**

**MDAI: FRIDA MWASA NDONDOLE**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: NDEBERYE BENJAMIN KITETE**

**TANGAZO**

Wewe **NDEBERYE BENJAMIN KITETE** popote pale ulipo unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani mnamo tarehe **31/5/2023** kama hutohudhuria basi Mahakama hii itasikiliza upande mmoja na uamuzi kutolewa.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SARAFINA ANOLD MTINDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye namba **PS02020281-276** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ULONGONI SHULE YA MSINGI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/169428/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**WAKURU LEAH JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.1502/2228** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HUNYARI SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **GEI/CHA/RB/1422697/2023.**



Mratibu wa Huduma za Afya kutoka Shirika la Standing Voice Tanzania, Innocent Mwandu (kushoto), akikabidhi vifaa saidizi vya kujikinga na mionzi ya jua kwa mmoja wa watoto wenye ualbino, Habiba Omary, kutoka Shule ya Sekondari ya Mlingano, Muheza mkoani Tanga juzi. Wa (pili kulia) ni Mratibu Msaidizi wa Shirika hilo, Ramadhan Mfinanga na (wa tatu kulia) ni Ofisa kutoka Shirika hilo, Robi Mataiga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Biashara zarejea rasmi Kariakoo

**Na Halfani Chusi**

HATIMAYE wafanyabiashara wa Kariakoo na maeneo mengine wameridhia kufungua maduka yao baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuahidi kutatua kero zao kwenye mkutano uliofanyika juzi, jijini Dar es Salaam.

Majaliwa alikutana na wafanyabiashara hao kwa mara ya pili ili kuwapa nafasi ya kusikiliza kero zao baada ya maagizo aliyoyatoa awali kupuuzwa, kisha baadaye alitatua kero sugu zilizokuwa zinalalamikiwa, ikiwamo ile ya usajili wa stoo na kufuta kikosi kazi.

Baada ya utatuzi huo, Majaliwa aliyekuwa akizungumza kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliwaomba wafanyabiashara hao kurudi kufungua maduka yao, jambo ambalo lilikubaliwa.

Mfanyabiashara wa simu Kariakoo, Mtaa wa Swahili, Malaki Msigala, alisema wamekubali ombi la Waziri Mkuu baada ya kutatua kero zilizokuwa zinawakabili.

"Waziri Mkuu jana (juzi) alifanya jambo kubwa sana. Ametatua kero zetu hapo hapo hicho ndio tulichokuwa tunahitaji.

Hatutaki siasa tunataka utekelezaji na yeye amelifanya hilo.

"Jambo lingine alikemea rushwa na kauli chafu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) dhidi yetu, ikiwamo ile ya kusema kauli ya Rais ni ya kisiasa mpaka waone barua rasmi na kamata kamata iliyo kinyume na sheria," alisema.

Mfanyabiashara mwingine wa Mtaa wa Swahili, Ajuza Musa, alisema serikali imerudisha furaha kwa wafanyabiashara huku akibainisha kuwa walikuwa wanateseka.

"Tumehangaika sana kupata haki yetu, sisi tunapenda kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yetu, lakini katika njia ya amani na usalama. Ukiona wafanyabiashara wanakubali kukaa juani kumsubiri Waziri Mkuu, ujue wamevumilia sana.

Hakuna mfanyabiashara ambaye anataka kukaa bila kuingiza fedha," alisema.

Mfanyabiashara Juma Zakaria alisema wamekubali kurejea kwenye maduka yao kwa sababu Waziri Mkuu ameunda tume jumuishi yenye wafanyabiashara na watu kutoka serikalini.

Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Uroki Ombeni, alisema wameridhishwa na uamuzi wa serikali akibainisha kuwa kwa sasa hawana shaka wanaamini utekelezaji wake utafanyika hata kwa yale ambayo hayakupatiwa ufumbuzi kwenye mkutano huo.

Nipashe pia ilishuhudia maduka mengi kwenye mitaa mbalimbali yamefunguliwa na wafanyabiashara wakiendelea na shughuli zao.

# Mshtakiwa aeleza kilichompeleka kwa DPP

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Joshua Kamalamo (39) ameieleza mahakama kuwa alikwenda ofisini kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, kwa ajili ya kumpelekea 'clip' ambayo ilikuwa inamzungumzia vibaya DPP aliyepita, Biswalo Mganga.

Kamalamo na Yahya Kapalatu wanadaiwa kujitambulisha mbele DPP Mwakitalu na Naibu wake, Joseph Pande, kuwa wao wametoka ofisi ya Rais na ni maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) kwamba wamepewa maelekezo kuwa kesi inayomkabili Habinder Sign Seth na wenzake isiendelee kusikilizwa.

Kamalamo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati akiongozwa na Wakili Method Kagoma kutoa utetezi wake katika kesi inayomkabili.

Mshtakiwa alidai kuwa Juni 11, 2021 alimpigia simu Pande baada ya kupewa namba yake ya simu na Biswalo kwa ajili ya kuomba kuonana naye.

Alidai kuwa baada ya kumpigia simu Pande, alijitambulisha na kumweleza kuwa namba yake alipewa na Biswalo kwa hiyo aliomba kuonana naye kwa ajili ya kumpeleka 'clip' hiyo. "Nilifanya hivyo baada ya Biswalo kuisikiliza kisha kunielekeza niipeleke kwa Naibu DPP wa sasa ili kama anaweza kuifanyia kazi," alidai Kamalamo.

Alidai kuwa Pande alimwuliza hiyo 'clip' inahusu nini na akamwambia ilikuwa inamweleza vibaya DPP. Alidai ilipofika saa 9:30 alasiri, Pande alimpigia simu kwa ajili ya yeye kupeleka klipu hiyo na alipofika ofisini kwake alitoa simu yake kwa ajili ya kumsikilizia, lakini bahati mbaya hakuiona.

"Niliposhindwa kuiona nilimweleza kuwa iko kwa bwana mdogo ambaye atamleta na kwamba 'clip' hiyo ilikuwa inahusu majadiliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi namba 27/2027 iliyokuwa inamuhusu Seth," alidai.

Kamalamo alidai baada ya kumweleza hivyo, alijibiwa kuwa ni bora na bosi wake mpya awapo na alijaribu kumpigia simu lakini hakupokea, hivyo alimweleza kuwa atafanya mawasiliano naye kisha atamjulisha ili afike ofisini na 'clip' hiyo.

Alidai siku hiyo usiku naibu huyo alimpigia simu kwamba tayari ameshazungumza na bosi wake, hivyo kesho awahi mapema saa 2:00 asubuhi na baada ya taarifa hiyo, alimpigia simu Kapalatu ambaye ndiye alikuwa na 'clip' hiyo.

Juni 12, 2021, alidai kuwa alikutana na Kapalatu kisha walikwenda pamoja ofisi ya DPP na walipofika akiwa na Kapalatu, waliingia ofisini kwa DPP kisha wakajitambulisha pamoja na muda huo alitoa simu akaiweka mezani na kisha akaichezesha 'clip' hiyo. "Clip' ilikuwa inasema Biswalo anajifanya mjanja hataki kuonana na sisi wakati tunataka kutengeneza mazingira ya kupata fedha, lakini yeye anajifanya mjanja. Kuna kitu tutatengeneza ambacho kitamletea shida kwa nafasi aliyo nayo kwa sababu anavyotukwepa utadhani tumechukuliana mwanamke," alidai Kamalamo.

Alidai kuwa Biswalo ni rafiki yake wa karibu sana pia ni jamaa yake na wanatoka sehemu moja, hivyo tayari alishamsikilizisha na baada ya kusikiliza hiyo mwenzake na DPP ambaye alikuwa pembeni akaanza kuuliza ninyi ni watu wa usalama, nikajibu hapana.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa washtakiwa walitenda makosa hayo Juni 11, 2021 katika ofisi za DPP zilizoko katika jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dar es Salaam na kujitambulisha kwa Pande ambaye ni Naibu DPP kuwa wametoka ofisi ya Rais na ni maofisa wa TISS.

# Tanzania na Uingereza kuboresha huduma afya

**Na Beatrice Shayo**

TANZANIA imetia saini mkataba wa ushirikiano na Uingereza kwa ajili ya kusaidia huduma za afya kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo utafiti, magonjwa ya milipuko na tiba.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe, wakati akizungumza na waandishi wa habari. Alisema watashirikiana na Uingereza kupitia diaspora ambao wako Uingereza kwa sababu ndio waliolianzisha suala hilo na kuishirikisha Wizara ya Afya.

Alisema ushirikiano huo unalenga katika maeneo ya utafiti, mafunzo, tiba na shughuli mbalimbali zinazohusisha afya na zitahusisha taasisi zao.

Kwa mujibu wa Shekalaghe, huo ni mkataba wa kwanza wa ushirikiano kati ya Wizara ya Afya na Uingereza na wamekuwa wakishirikiana kwa muda mrefu bila kuwa na makubaliano ya mkataba kama waliyofanya jana.

Pia alisema jambo jingine ambalo liko katika majadiliano na balozi amekubali kulifanyia kazi ni Uingereza kuingia katika mfuko wa pamoja ambao kuna nchi mbalimbali ambazo zinachangia kuwezesha kutoa huduma hasa katika afya ya msingi.

Alisema mazungumzo tayari yameshaanza na tayari wameshaandaa timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Afya ambao watakutana na wataalamu walioopo kwenye balozi ili kuhakikisha na Uingereza nayo itakuwa ni mojawapo kuchangia.

Katibu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Fatma Mrisho, alisema watafaidika katika utafiti, maeneo ya huduma za afya kuanzia ngazi ya chini hadi daraja la juu na kujenga miundo ambayo itawasaidia kuendesha huduma zao kwa ubora zaidi.

Alisema Zanzibar imekubaliana kuwapo bima ya afya kwa wote, hivyo wataomba kusaidiwa katika hilo ili kila mmoja aweze kupatiwa huduma za afya.

Mrisho alisema jambo jingine wanalolitegemea katika makubaliano hayo ni kuwapeleka wataalamu kwa ajili ya kusoma ili kujenga uwezo wao uwe wa juu zaidi na kupatiwa vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kuboresha huduma.

Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, alisema mkataba huo utachangia zaidi katika magonjwa ya kuambukiza, yasiyo ya kuambukiza na magonjwa ya mlipuko.

Alisema watachangia katika masuala ya dawa, utafiti na msaada huo ni kwa ajili ya Tanzania na Zanzibar.

Concar alisema wanafikiria namna ya kuanza kuchangia katika mfuko wa pamoja wa afya.

# Mkenda akemea uhamishaji wanafunzi holela wanapofeli

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuna baadhi ya shule binafsi zina matawi mawili ambayo mtoto akifeli anahamishiwa kwa nguvu tawi lingine.

Mkenda aliyasema hayo juzi bungeni jijini hapa wakati akihitimisha hoja za wabunge waliochangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge ikiwamo iliyohusu serikali imekuwa mshindani wa shule binafsi ndiyo maana ikaondokana na mfumo wa kutangaza kumi bora katika matokeo ya mitihani, alisema bado wanatoa madaraja na kuhoji kwamba huo si ushindani.

"Tunachosema lazima ushindani utegemee kigezo kinachokubalika. Kushindanisha shule ni tofauti na kushindanisha mwanafunzi. Kwani Kenya haipendi sekta binafsi mbona imefuta kutoa shule bora, Uganda je, UK je? Tutaangalia vigezo bora vya kushindanisha shule siyo vigezo kwamba wewe wanafunzi wanafanya vizuri sana wewe ni shule bora," alisema.

Alisema shule iliyochukua wanafunzi wenye daraja C na B halafu wote wakatoka daraja A na nyigine ikachukua wote wa daraja A wakatoka wote A ipi itakuwa bora. "Mnafahamu kuna shule zina matawi mawili, moja huku anayefeli anahamishwa kwa nguvu, mzazi hapewi nafasi ya kuchagua. Mtoto ameugua inatakiwa shule imlee, imsaidie badala ya kumsaidia inakutoa ili wabaki kupata daraja A ushindani huu hauna afya," alisema.

Akijibu hoja ya mbunge wa Songwe, Philip Mulugo, kuhusu uwapo wa mitihani mingi kila mwezi inayoanzia kata ambayo inazilazimisha shule binafsi kuishiriki kwa kuchangia Sh. 100,000, Waziri Mkenda alitangaza kuanzia sasa shule binafsi hazitalazimishwa kuifanya bali zitashiriki kwa hiari.

Kuhusu hoja za baadhi ya wabunge kwamba serikali inaichukulia sekta binafsi ya elimu kama mshindani wake, Prof. Mkenda alisema: "Hapana, haijawahi kutokea na haitatokea na haiwezi kutokea chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na haitatokea baadaye. Hii ni serikali ya wananchi, shule zinafundisha Watanzania," alisema.

"Shule binafsi pamoja na vyuo vikuu vimekuwa msaada. Tulikuwa tunaona watoto wetu wanaondoka kwenda Kenya au Uganda kusoma, leo shule zimetufuata nyumbani, tunazifurahia na kuzilinda," aliongeza.


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY CO. LTD**

OPEC FUND

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTANCY SERVICES**

**CONSULTANCY SERVICES FOR CONSTRUCTION SUPERVISION AND MANAGEMENT OF THE PROPOSED 220kV BENACO-KYAKA TRANSMISSION LINE, SUBSTATION AND RURAL ELECTRIFICATION IN KAGERA REGION, TANZANIA**

**Tender No. PA/001/2022-23/HQ/C/10**

The Government of the United Republic of Tanzania (GoT) has applied for financing from OPEC Fund for International Development (OPEC Fund), Abu Dhabi Fund for Development (ADFD) and Saudi Fund for Development (SFD) towards cost of 220kV Benaco-Kyaka Transmission Line and Substation and intend to apply part of the agreed amount for this credit to payments under the contract for Provision of Consulting Services for Supervision and Management of the Benaco-Kyaka Transmission Line Project.

The services under this project will entirely include and not limited to the following;

a) Review of project documents including tender documents, RAP, ESMP, engineering studies and design based on 2021 Feasibility study;
b) Review and approval of detailed and final engineering design of the project prepared by the EPC contractors to ensure technical soundness prior to implementation of works;
c) Control and Supervision of the EPC contractors;
d) Carrying out supervision of works to ensure compliance with the approved Designs, Drawings, Specifications, Contracts, Tanzania Grid codes, schedule of work and best Engineering practice;
e) Supervision of the Project's Environmental and Social Management Plan;
f) Coordination of project activities of all parties executing the project to achieving the planned implementation schedule;
g) Preparation of Inception Report;
h) Assistance to TANESCO during procurement processes (advertisement, clarification, site visit, evaluation and contract negotiations);
i) Assistance to TANESCO in Planning and Coordinating of RAP implementations and ESMP activities;
j) Assistance to TANESCO in establishing, reviewing and monitoring timeline for project implementation;
k) Prepare update time schedule for the project (consultant services as well as the implementation project);
l) Supervision of correction for defects under all contracts;
m) Collation and preparation where appropriate of Operations and Maintenance manuals, as-built drawings and other design/construction records;
n) Coordination of monitoring of RAP and ESMP activities;
o) Preparing and submitting periodic and other reports to TANESCO;
p) Approval of issuance of acceptance and completion certificates;

The consultant will be stationed where most of the administration works will be conducted. During Phase 2 Construction stage of the project the consultant will be stationed in Kagera at the project site. The Project is planned to be implemented in Two (2) years from the contract commencement date.

Tanzania Electric Supply Company (TANESCO) Ltd, the project implementation agent, now invites eligible Consultants to indicate their interest in providing these services.

The Interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, company profile and financial status, etc.).

For the purpose of demonstrating experience in the **expression** of interest, Consultants should list **at least three (3)** and **at most ten (10)** successful project implementation experiences in the items indicated below:

- General Experience of Consultant in Transmission Line, Substation and Distribution Projects of the similar size and nature or above not less than fifteen (15) years
- Specific Experience of Consultant in Design and Supervision of Transmission line, Substation and Distribution projects, Transmission Lines and Substations not less than ten (10) years;
- Technical and Managerial Organization of the Firm;
- Experience of the Consultant in sub-Saharan Africa

Consultants may constitute joint-ventures to enhance their chances of qualification.
Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the OPEC Fund/Tanzania Procurement Guidelines.

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours 09.00 – 12.30 hours and 14.00 – 16.30 hours local time (Monday to Friday) excluding public holidays.

The interested Potential Consultants have option either to submit physically as per address below and **mention "Expressions of Interest for Provision of Consultancy Services for Supervision and Management of the 220kV Benaco-Kyaka Transmission line, Substation and Rural Electrification". This Bids will be opened on 23rd June 2023 at 10:30 hours East African Time;"**

**Attn: The Secretary-Tender Board,**
**TANESCO Umeme Park Building, Ubungo,**
**Ground Floor, Tender Room, Room No. G04,**
**P.O. Box 9024,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: 255 (22) 2451145/2452172; +(255) 782 376147**
**Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz**
**pmuprojects@tanesco.co.tz;**

**Managing Director,**
**Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jukumu la kulea familia lisiachwe upande mmoja

**WAKATI** jana ikiwa Siku ya Familia, jamii inakumbushwa kuwa jukumu la kulea familia linahusu pande zote.

Mke na mume wanapoamua kuanzisha familia, wote kwa pamoja wanapaswa kupanga jinsi ya kulea familia yao kwa kushirikiana.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwapo na tabia ya wanandoa kuachiana mzigo wa kulea watoto kuanzia chakula, mavazi mpaka ada za shule. Mara nyingi jukumu hilo huachiwa mwanamke na kubebeshwa mzigo mkubwa wa kulea familia.

Tabia hiyo imeelezwa kuwa ni chanzo kimojawapo cha watoto kukosa maadili mema katika jamii.

Mama au baba anapoelemewa na majukumu wakati mwingine hushindwa kufuatilia mienendo ya watoto wao.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa katika maadhimisho ya Siku ya Mama Duniani jijini Dar es Salaam juzi, ambayo yalienda sambamba na uzinduzi wa taasisi ya Binti Lindi Initiative, alisema ni muhimu wazazi waangalie na kufuatilia kwa karibu mienendo ya watoto wao ikiwamo tabia zao na maendeleo yao shuleni na kuwa karibu na walimu.

Aliwasihi kinababa kuacha kukimbia majukumu na malezi kwa watoto wao na kuwachia wanawake peke yao kwa kuwa kufanya hivyo kunachangia kwa asilimia kubwa mmomonyoko wa maadili na vitendo vya ukatili kwa watoto.

"Niwaombe wanaume wenzangu chondechonde suala la maadili linaelekea pabaya watoto wetu wanaharibika, jahazi linazama, hivyo tuondokane na kuwaachia wake zetu malezi, tunakabiliwa na tatizo la mmomonyoko, tubadilike."

Kauli hiyo ya Waziri Mkuu inakumbusha jinsi sasa hivi maadili yalivyoporomoka ya watoto kuharibika na kujiingiza katika utamaduni ambao hapo zamani haukuwapo nchini.

Kutofuatiliwa kimalezi, watoto wanaingia katika wimbi la kuiga maisha ya mitandao yanayoonyesha watu kumiliki majumba ya kifahari au kuwa na magari mazuri bila kufikiri kuwa wakati mwingine hayo ni maisha ya maigizo.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Khamisi, akizungumzia hali hiyo, alisema tayari wameshaunda madawati maalumu ya watoto katika shule za msingi na sekondari ili waweze kuripoti vikwazo vinavyowakabili watoto wanapokuwa huko.

Wengine huogopa kuwasiliana na wazazi wao kwa hofu ya kupigwa au kutishiwa na watu wanaowafanyia vitendo hivyo.


Alisema watoto wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo vingi vya kimalezi huku wakiwa hawana pa kusemea, na kwamba wizara imeona ianzishe madawati hayo, ili kuwafikia kirahsi.

"Wazazi kwa pamoja tushirikiane katika malezi, ili kupata jamii bora, kwani jukumu la malezi ni letu sote, asiwepo wa kukimbia majukumu na kumwachia mwingine."

Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Lindi, Kijakazi Yunus, katika kupigia msumari suala hilo anakumbusha kuwa malezi ni jukumu la watu wote kuanzia ngazi ya familia, jamii hadi taifa na kwamba kwa ushirikiano huo ni rahisi kutatengeneza taifa bora.

Jamii ione umuhimu wa kuangalia watoto bila kujali umemzaa wewe. Tukumbuke wazee wetu walivyokuwa wakiwalea watoto hata kama sio wa kwake akiona amekwenda kinyume na maadili atamkanya na kumripoti kwa mzazi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kumlea mtoto kinababa punguzeni 'ubize muwajibike, mliobaki nanyi inawagusa

Na Pilly Kigome

**KUNA** usemi usemao samaki mkunje angali mbichi hii ina maana ya kuwa mtoto angali bado kijana mdogo, ndio anatakiwa aelekezwe na kupandikizwa tabia zilizo njema na mzazi au mlezi, pasipo kufanya hivyo, baadae kunaweza kumsababishia aonekane ni mtu wa ajabu katika jamii, kwa kuwa muda wa kumkunja na kumjenga umekwisha.

Ni usemi unaoenda sambamba na ule wa 'mtoto umleavyo ndivyo akuavyo'. Na hii ni kweli tupu zaidi ya asilimia 99, kwa kuwa mzazi au mlezi ndio mzizi wa tabia za mtoto wake.

Nafikiri hakuna anayebisha usemi huu kwakuwa tumeona ama kusikia yakuwa baadhi ya watoto katika jamii wamekuwa na mienendo kinyume na maadili kutokana na kukosa malezi ya mzazi au mlezi, ambayo yalishindwa kumjenga hapo awali akiwa bado yu kijana mdogo.

Hivyo, katika suala zima la maadili kwa watoto wetu ni suala la kushirikiana kwa pamoja baba na mama ikiwemo na jamii kwa ujumla ili kutengeneza taifa lenye watu makini.

Suala la malezi si la wazazi pekee, lakini asilimia kubwa maadili yanaanzia ndani ya familia, ndipo inafuata jamii wao nao wanahusika kwa namna moja au nyingine katika kuwajenga watoto wetu.

Kumekuwa na mabadiliko ya maadili katika jamii yetu, mzazi anakuwa mtu pekee anayeweza kumuadhibu, pindi anapokosea. Ni mzazi au mlezi pekee, hilo jambo amekuwa nalo linaleta mkanganyiko katika jamii. kwakuwa watoto wamekosa mwongozo kutoka kwa walezi wao.

Nakumbuka miaka ya nyuma wakati sisi tunakua, ilikuwa mtu yeyote mkubwa aliyekuzidi umri huwa mzazi wa mwenzako, anakuwa na uhuru wa kukuadhibu pindi anapokukuta umekosea na umekuwa unakubali adhabu hiyo.

Kwa bahati mbaya, pindi unapoenda nyumbani ukionekana aidha unalia au unasimulia tukio hilo lililokukuta huko ulikotoka, basi mzazi naye anaongezea pale alipoishia mwenzake, kwa kukuongezea adhabu pasipo kumfuata yule aliyekuadhibu na kukubali mwanangu adhabu aliyopewa inastahili.

Miaka hii imekuwa kinyume, kwa kuwa huwezi kumuadhibu mtoto asiyekuwa wako ukifanya hivyo basi unaanzisha ugomvi au matatizo na mzazi mwenzako, kwa madai ya kuonekana umefanya kitendo cha ajabu cha kumuadhibu mtoto wake pasipo yeye kuwepo au kumpa ridhaa.

Hata hivyo, walezi wengi wamekuwa wakikutana na changamoto za Watoto hao kuadhibiwa na mtu mwingine ambaye si mzazi wake na kama mtoto huyo maadili ni mabaya zaidi, anaweza akakuongeza na matusi na kukuumbua mbele za watu ama kukudhalilisha kukataa kuadhibiwa kwakuwa hujamzaa wewe.

Ndipo tunapoona siku hadi siku mmomonyoko wa maadili unazidi kukua kwa watoto wetu kutokana na kufumbia macho na kutokuchukua hatua stahiki kwa watoto wetu pindi wanapoonekana wanaenda kinyume.

Mbali na hilo, pia tumeona malezi yamekuwa yakiwaelemea wazazi wa kike pekee na wazazi wa kiume kutingwa na 'ubize' wa ama kupitiliza au kujiondoa katika suala la malezi. Hili nalo ni chanzo cha kuwafanya watoto wetu kukosa maadili yaliyomema.

Hivi karibuni tumemsikia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, katika siku ya maadhimisho ya Siku ya Mama Duniani, yaliyoandaliwa na taasisi ya Binti Lindi, akiwa anawakumbusha kinababa kutokukwepa majukumu ya malezi kwa watoto wao.

Anasema, kinababa wanapokwepa majukumu yao ya kimsingi majumbani, nako kunachangia kwa asilimia kubwa kuzalisha watoto wanaokosa maadili na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili katika jamii.

"Nawaomba kinababa wenzangu, chondechonde tusikimbie majukumu kuwaachia akinamama pekee, tupunguze 'ubize', tusimamie mienendo ya watoto wetu majumbani na shuleni, ili tuzalishe na kupunguza ama tuondoe kabisa mmomonyoko wa maadili kwani tuko katika kipindi kigumu ndugu zangu" akawakumbusha wanaume.



Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya Absa Tanzania, George Binde (wa nne kushoto), akikabidhi baadhi ya vifaa vya hospitali kwa Mratibu wa Magonjwa yasiyoambukiza wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dk. Milka Mathania, vilivyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja juzi, ili kusaidia juhudi za serikali katika kuboresha huduma za afya nchini hususan kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha tukio la Absa Dar City Marathon lililogharimu Sh. milioni 45. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne kati ya 10 mikoa 7 wana BP

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema watu watatu hadi wanne kati ya 10 wana shinikizo la juu la damu katika mikoa saba ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mikoa hiyo iliyobainika baada ya kufanyiwa uchunguzi wa jamii ni Pwani, Arusha, Geita, Mtwara, Lindi, Iringa Dar es Salaam na Zanzibar.

Aidha, wagonjwa sita kati ya 10 wanaoonwa kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wana ugonjwa huo.

Mwalimu alibainisha hayo jijini hapa juzi wakati akitoa tamko kwenye maadhimisho ya siku ya shinikizo la juu la damu duniani yaliyoambatana na kaulimbiu: 'Pima shinikizo la damu kwa usahihi, idhibiti, ishi kwa muda mrefu.

Alisema kwa wagonjwa waliotibiwa JKCI tangu ilipoanzishwa Septemba 2015 hadi Aprili 2023 kati ya wagonjwa 619,102 waliotibiwa asilimia 66 ya wagonjwa walikuwa na tatizo la ugonjwa huo.

Alibainisha kuwa shinikizo hilo linasababisha kiharusi, shambulio la moyo, moyo kushindwa kufanya kazi, kutuna kwa kuta za mishipa ya damu, moyo, uharibifu kwenye chujio za figo, ganzi miguuni na mikononi, upofu na kupunguza nguvu za kiume.

Waziri huyo alisema serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, inaendelea na utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007, ambayo inalenga kutoa huduma kwa magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo ugonjwa wa shinikizo la juu la damu kwa umahiri zaidi.

Alisema, huduma za matibabu ya shinikizo la juu la damu zimekuwa zikitolewa na vituo vyote vya afya nchini kuanzia ngazi ya vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufani za Mikoa na Kanda na Hospitali Maalum.

Alisema katika mkakati wa kuboresha huduma hizi serikali imeendelea kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kwa kuboresha miundombinu na vifaa tiba, kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kuwatambua, kuwaibua na kuwahudumia wagonjwa wa shinikizo la juu la damu.

Hata hivyo, alisema mpango wa serikali kupitia Wizara ya Afya ni kutoa mafunzo ya utoaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo huduma za ugonjwa wa shinikizo la damu kwa watoa huduma 2,400 kutoka vituo vya afya vyote 600 katika mikoa yote 26.

Alisema mpaka sasa wizara imekwishatoa mafunzo hayo kwa jumla ya watoa huduma 1972 kutoka mikoa 19 kati ya 26 ambayo ni sawa na asilimia 73, yanayotarajiwa kukamilika kufikia mwezi Juni, 2023 na wizara imetoa vifaa vya utambuzi wa awali vya magonjwa hayo kwa vituo vya afya kwenye mikoa hiyo.

"Wizara imeruhusu dawa za kukabili shinikizo la juu la damu katika ngazi ya msingi kwa kuruhusu dawa tatu kutumika katika ngazi ya kituo cha afya na dawa mbili kutumika katika ngazi ya zahanati," alisema.

# EPZA yaita wafanyabiashara kuwekeza maeneo saba nchini

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji nchini (EPZA), imeita wawekezaji wenye nia ya kuanzisha viwanda ili waendeleze maeneo saba yaliyopo katika mikoa ya Mbeya, Lindi, Dar es Salaam, Tanga na Shinyanga, chini ya utaratibu wa mamlaka hiyo.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, kwa vyombo vya habari jana ilitaja maeneo yaliyopo Dar es Salaam kuwa ni vitalu namba 184/185 na 186/185 ambazo ni jumla ya ekari 8.39, zilizopo eneo la viwanda Chang'ombe, katika Manispaa ya Temeke, zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa kampuni ya taifa ya chuma.

Lingine kwa Dar es Salaam ni mita za mraba 15,000 zilizopo eneo Maalum la Kiuchumi la Benjamin William Mkapa, Mabibo External, ambalo ni maalumu kwa shughuli za kibiashara.

Mkoani Tanga, EPZA imetangaza shamba namba 11 lenye ukubwa wa ekari 36, lililopo Kijiji cha Mkata, kando ya barabara ya Mkata-Handeni, takribani kilomita moja kutoka makutano ya barabara ya Dar es Salaam-Tanga, wilayani Handeni.

Kwa mujibu wa Itembe, mkoani Lindi kuna maeneo mawili ambayo ni ekari 9.97 zilizokuwa za kiwanda cha korosho Wilaya ya Nachingwea na ekari 9.81 zilizokuwa kiwanda cha kusindika mafuta ya ufuta wilayani humo.

Katika mikoa ya Shinyanga na Mbeya, EPZA imetangaza ekari 1431.62 za maeneo yaliyokuwa yanamilikiwa na kampuni ya Tanganyika Packers.

Mgawanyo wa maeneo hayo ni ekari 1179.23 lililopo Mwalugoye Shinyanga na ekari 252.39 zilizopo barabara ya Chunya, Mbalizi.

"Maeneo yote yanafikika kwa barabara na yana huduma zote muhimu kama umeme na maji," alisema Itembe katika taarifa hiyo.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed





Watendaji mbalimbali (kutoka kushoto) ni Mtendaji Mkuu wa ALP Afrika Mashariki, Francis Gimara, Mkuu wa Maudhui na Ujuzi ALP Afrika Mashariki, Herry Onoria, Msajili EACJ, Christine Mutimura, Mmoja wa wamiliki wa ALP Nigeria, Solagbade Sogbetun, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Herman Kasekende na Mkurugenzi wa Leaf Tobacco and Commodities, Claude Ndahangarwa, wakionyesha ripoti ya Huduma na Bidhaa za Afrika ya Mashariki katika soko la pamoja la Afrika ya Mashariki, baada ya kuzinduliwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Hakuna kipindupindu Mabwepande'

**Na Jenifer Gilla**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amesema hakuna maambukizi ya ugonjwa wa kipindupindu katika Kata ya Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, kama inavyoaminika kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo.

Kauli hiyo imekuja baada ya kuenea kwa taarifa kutoka kwa watu wanaoishi maeneo hayo kuwa ugonjwa huo umeenea katika kata hiyo, hali iliyozua taharuki kwa wakazi wake na kata za jirani.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk. Mfaume alisema kinachotokea katika eneo hilo ni hofu iliyotengenezwa na watu baada ya kuona maofisa afya wakisafisha moja ya nyumba iliyokuwa na mtoto aliyehisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Alisema wiki moja iliyopita Hospitali ya Wilaya Mabwepande ilipokea mtoto aliyekuwa na dalili za ugonjwa huo, baada ya kupatiwa matibabu na kuruhusiwa kurudi nyumbani maofisa afya walikwenda kusafisha nyumba anayoishi ili kuzuia maambukizi kwa wengine.

"Kwa hiyo watu walipata taharuki baada ya kuona gari la wagonjwa katika nyumba hiyo na kisha maofisa afya wakisafisha kwa dawa, lakini ukweli ni kuwa hakuna mgonjwa yeyote wa kipindupindu aliyeripotiwa mpaka sasa katika kata hiyo," alibainisha.

Aidha, alisema hakuna mgonjwa mpya aliyeripotiwa katika mkoa huo tangu kutangazwa kulipuka kwa ugonjwa huo Aprili 25, mwaka huu na Wizara ya Afya, baada ya watu 15 kubainika kuugua, 13 wakitokea Wilaya ya Ilala na wawili Wilaya ya Kinondoni.

Alitaja maeneo yaliyothibitika kuwapo na maambukizi ya ugonjwa huo mpaka sasa kuwa ni Kivule, Tabata Dampo, Kinondoni na Buguruni.

Alisema timu ya maofisa afya inafanya kazi kubwa ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo, ikiwamo kumwaga dawa ya kuua vimelea kwenye makazi ya watu.

Akitoa taarifa za ugonjwa wa Margbug Aprili 30, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ya kuwapo ugonjwa wa kipindupindu, jijini Dar es Salaam.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchukua tahadhari ikiwamo kutibu maji kwa kutumia dawa ya kuua vijidudu ya Chlorine au kuchemsha maji ya kunywa, kuepuka kula chakula kilichopoa, kunawa na maji tiririka na sabuni na kuosha matunda kabla ya kula.

Aidha, aliwataka wanaotiririsha majitaka kutoka vyooni waache mara moja kwa kuwa yanachangia kuenea ugonjwa huo kwa kasi.

# Wakazi Vikuruti kunufaika ujenzi zahanati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI 4,200 wa Vikuruti Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, wanatarajia kuondokana na kero ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya baada ya ujenzi wa zahanati iliyojengwa kwa fedha za halmashauri na wananchi Sh. milioni 152.

Hayo yamebainishwa na Mganga Mkuu wa Halmashauri wilaya hiyo, Wilford Kondo alipokuwa akitoa taarifa wakati Mwenge wa Uhuru ulipopita kukagua na kuweka jiwe la msingi katika zahanati hiyo.

Dk. Kondo alisema, awali wananchi hao walikuwa wakitembea kilomita sita kufuata huduma za afya na sasa ujenzi wa zahanati hiyo umefikia asilimia 85.

Alisema lengo la mradi huo ni kusogeza huduma karibu na wananchi huku kaya 840 katika kitongoji cha Vikuruti na vingine vya jirani vikitarajiwa kunufaika na zahanati hiyo.

Dk. Kondo alibainisha kuwa kati ya fedha hizo, Sh. milioni 150 ni mapato ya ndani ya halmashauri na Sh. milioni 2.5 zilitokana na nguvu za wananchi.

Mwajuma Issa, mkazi wa Vikuruti aliishukuru serikali kwa kufanikisha ujenzi wa zahanati hiyo ambayo itawapunguzia usumbufu waliokuwa wakikumbana nao awali wanapohitaji huduma za afya.

Akitoa taarifa baada ya kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya ya Bagamoyo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Saimon, alisema Mwenge huo utakimbizwa katika miradi 14 ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha yenye thamani ya Sh. trilioni 3.1.

# Tz, Japan zakubaliana kujengea uwezo wataalamu gesi asilia

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Nishati pamoja Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), wamesaini makubaliano ya kutekeleza mradi wa kujengea uwezo wataalamu wa wizara na taasisi zake katika eneo la kuendeleza matumizi bora ya gesi asilia ili kuiwezesha Tanzania kuendelea kunufaika kiuchumi na rasilimali hiyo.

Makubaliano hayo yamesainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba na Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania, Ara Hitoshi, Mei 16, 2023, jijini Dar es Salaam.

Makubaliano hayo yatawezesha wataalamu wa Tanzania kuongeza ufanisi katika kufanya mipango na kutekeleza miradi ya matumizi ya gesi asilia kwa kuzingatia pia suala la utunzaji wa mazingira.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kushoto), akizungumza na wakazi wa Kata ya Naberera, katika ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Filamu ya The Royal Tour yazidi kuleta neema watalii

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, amesema idadi ya wageni walioitembelea Tanzania tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipozindua filamu ya 'The Royal Tour' imefikia watalii milioni 1.7

Alitoa taarifa hiyo jana katika Uwanja wa Ndege wa Arusha, baada ya kupokea ujumbe wa watu 40 kutoka nchini China.

Mchengerwa alisema serikali imepanga kufanya nao vikao mbalimbali na kujadili hali ya uwekezaji katika utalii.

Ujumbe huo unaojumuisha mawakala wa utalii, waandishi wa habari na watu wenye ushawishi kutoka China, wako nchini kuanzia Mei 11 hadi Mei 23 mwaka huu, chini ya uratibu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Kamisheni ya Utalii Zanzibar.

Ujumbe huo utatembelea mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Zanzibar na Dar es Salaam.

"Tumewapokea wageni wetu, lakini tutakuwa na vikao nao. Watatembelea maeneo mbalimbali na vivutio vyetu. Tutajadili hali ya uwekezaji, tunapozungumza idadi ya watalii imeongezeka na hivi karibuni tutatoa takwimu. Mpaka sasa tumewafikia watalii milioni 1.7 na tunaelekea milioni 1.8,"alisema Mchengerwa.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Anderson Mutatembwa, alisema serikali inaendelea kufanya uratibu wa karibu ingawa tatizo kubwa lililoko kwa sasa ni kupungua kwa miundombinu wezeshi ya kuhudumia watalii.

"Mheshimiwa Waziri ametoa baadhi ya takwimu, kwa mfano kwa Ngorongoro, kiwango cha juu kabisa ambacho wameweza kukipata cha mapato kilikuwa Dola zaidi ya milioni 140, lakini mpaka mwezi uliopita, wameshavuka lengo mpaka kufikia Dola milioni 160.

"Hii ni moja ya matunda makubwa sana ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika filamu ya The Royal Tour. Tatizo tulilonalo sasa hivi ni katika kuendelea kujenga miundombinu wezeshi, ikiwamo hoteli na tunafanya hivyo kwa kushirikisha wadau, lakini na bidhaa nyingine ambazo ni mtambuka ambazo tuna uhusiano nao," alisema.

Aidha alisema hivi karibuni, Wizara ya Maliasili na Utalii itatoa muongozo wa uwekezaji ambao utabainisha fursa za uwekezaji katika maeneo mawili.

Alisema mojawapo ni eneo la ndani ya hifadhi ambalo serikali itabainisha maeneo kwa kushirikiana na halmashauri za maeneo ambayo yanapakana na maeneo ya hifadhi ili na zenyewe ziandae matumizi bora ya ardhi, kwa ajili ya kuendelea kuvutia maeneo yetu ya uwekezaji.

Mwakilishi wa Ubalozi wa Tanzania nchini China, Dk. Miraji Ussi, alisema: "Tumechanganya makundi hayo kwa sababu tunataka kuongeza visibility ya Tanzania nchini China, lakini tunataka bidhaa za Tanzania ziuzwe nchini China."

## Prof. Ndalichako atoa maagizo vyuo vya ufundi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ameagiza vyuo vya ufundi kujikita kutoa mafunzo yatakayomwezesha mhitimu kuwa na ujuzi.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha alipotembelea mabanda ya maonyesho ya Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Standi (NACTVET).

"Nimepata fursa ya kutembelea mabanda ya vyuo vikuu, vyuo vya kati na vile vya ufundi stadi vinavyotoa mafunzo mbalimbali na nimeona namna walivyojipanga katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo. Pia nimeona wanatumia vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli zao.

Alisema kwa sasa mwelekeo wa serikali ni kuhakikisha kwamba mitaala ya elimu inalenga kukuza ujuzi kwa wanafunzi ambao utawaongezea maarifa na itawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Dk. Adolf Rutayuga, alisema maonyesho hayo yanafanyika kwa mara ya tano na wamekuwa wakivikutanisha vyuo hivyo na wadau ili kuwaonyesha Watanzania shughuli wanazofanya ikiwamo teknolojia wanazogundua na mafunzo yanayotolewa.

Vilevile alisema kwenye maonyesho yatakuwa na washiriki 160 ambao wana vibanda lakini kwenye kongamano wako washiriki zaidi ya 300.

Washiriki wa maonyesho hayo, akiwamo Pascal Marusu ambaye ni Mkuu wa Idara Famasia kutoka Chuo cha Sayansi za Afya cha Kolandoto, alisema kupitia maonyesho hayo, watapata fursa ya kuonyesha watu teknolojia ya hali ya juu na mafunzo kwa vitendo wanavyowafundisha wanafunzi kwenye chuo hicho.

# Nchi 38 kushiriki maonyesho ya kimataifa Karibu-Kili Fair

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATALII kutoka nchi zaidi ya 38 duniani wamethibitisha kushiriki maonyesho ya kimataifa ya Karibu-Kili Fair na kutembelea vivutio mbalimbali nchini.

Maonyesho hayo yanatarajia kufanyika kuanzia Juni 2 hadi 4 mwaka huu mkoani hapa.

Akizungumza jana jijini Arusha, Mkurugenzi wa Kilifair Ltd ambao ndiyo waandaaji wa maonyesho hayo, Dominic Shoo, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutangaza vivutio vilivyopo nchini.

"Kila mwaka tumekuwa na ongezeko la wadau hawa kutoka nchi mbalimbali duniani kwa sababu ya Filamu ya The Royal Tour, aliyofanya Rais Samia Suluhu Hassan, lakini na sisi kupitia onyesho hili tunalofanya kila mwaka imetusaidia kuitangaza nchi hivyo dunia inafahamu Tanzania,"alisema.

Alisema onyesho hilo litakuwa la kipekee baada ya dunia kukumbwa na janga la ugonjwa wa virusi vya corona kwani itatoa fursa ya njia za kuzifuata katika sekta ya utalii ili wadau wazifahamu na kupiga hatua zaidi ya hapo walipo.

"Katika maonyesho haya pia tunatarajia kampuni zaidi ya 370 kutoka nchi zaidi ya 12 duniani, wamejiandikisha kushiriki onyesho hili na pia kupitia onyesho hili ni fursa ya nchi kujiuza kwenye nchi jirani juu ya vivutio vyetu," alisema.

Vile vile alisema kupitia onyesho hilo wanalofanya kila mwaka wamefanikiwa kuleta watu zaidi ya 500 kutoka mataifa mbalimbali duniani ambao wanaamini wamekua mabalozi wazuri wa kutangaza vivutio vilivyopo nchini.

Ofisa Mkuu wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema wao pia ni miongoni mwa wadhamini wa maonyesho hayo na kila mwaka wanashiriki wakiamini sekta ya utalii ni mojawapo inayoingizia mapato makubwa taifa.

"Kwa takwimu za mwaka jana za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilisema sekta hii ilikuwa ya pili baada ya madini kwa kuingizia taifa Dola za Kimarekani bilioni 2.4 hivyo vizuri kusaidia wadau wazidi kusonga mbele kwa manufaa ya nchi yetu," alisema.

Raballa alisema katika kipindi cha ugonjwa wa virusi vya corona benki yao walihakikisha wanainua wafanyabiashara wa sekta ya utalii kwa kuwapa mikopo ya magari, lengo likiwa hawakwami kutoa huduma bora kwa watalii wanaofika nchini kuangalia vivutio mbalimbali.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wakala wa Utalii Tanzania (TATO), Henry Kimambo, alisema lengo la kukutanisha wadau wa utalii wa ndani na nje ya nchi, ili kufanikisha azma ya serikali ya kufikisha watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025.





# Wakurugenzi CPB wapewa mafunzo ya uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAKURUGENZI wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) wamepewa mafunzo ya uongozi ya utawala bora na Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania (IoDT).

Akizungumza baada ya mafunzo hayo Mwenyekiti wa CPB, Salum Awadh, alisema mafunzo yatawawezesha kufanya kazi kwa mafanikio.

"Kwenye mashirika ya umma kuna matatizo ya kiuongozi ya kusimamia mali za umma, hivyo ukiwa na uwezo mdogo huwezi kusimamia rasilimali, kwa hiyo mafunzo haya yatasaidia wakurugenzi wa bodi kuelewa mipaka yao," alisema.

Alisema mafunzo hayo yanasaidia kuonyesha mipaka kati ya bodi na menejimenti, hivyo mafunzo haya yamekuja wakati mwafaka.

Aidha alisema awali bodi hiyo ilikuwa ikifanya kazi zake kwa ufanisi mdogo lakini katika msimu huu bodi hiyo imepanga kuboresha ufanisi wake kwa kuchakata mazoa zaidi ya tani 200.

Awadh alisema katika kipindi cha nyuma katika upande wa viwanda walikua hawafanyi vizuri hivyo sasa wamejipanga kufanya kwa ufanisi kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 70.

Mmoja wa wajumbe wa bodi hiyo, Kapenjama Ndile, aliongeza kuwa mafunzo haya yatawasaidia kuendesha mashirika ya umma kwa kuongeza uwezo wa kiulewa wa namna ya kuendesha mashirika ya umma hasa katika sekta ya kilimo.

Ndile alisema kuwa bodi hiyo ipo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na kukuza uchumi wa nchi, hivyo taasisi yao itanunua mazao mengi na kuyachakata katika viwanda vya CPB .

Mjumbe mwingine wa bodi hiyo, Halima Dendego, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kujiimarisha, wanapata ujuzi ili wajiendeshe kiushindani.

Taasisi ya IoDT imekuwa ikitoa mafunzo hayo kwa wakurugenzi wa taasisi mbalimbali za umma wakiwemo wakurugenzi wa CPB.

CPB ni shirika la umma la kibiashara lililopo chini ya Wizara ya Kilimo ambalo ununua mazao kutoka kwa wakulima na wafanyabiashara wa mazao na kuyaongezea thamani kwa kuyachakata katika viwanda vyao vilivyopo katika baadhi ya mikoa.

# Viongozi sekta ya afya chanzo ubovu wa huduma

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KATIBU wa Chama cha Makatibu wa Afya Tanzania, Juliana Mawala, amelalamikia tabia ya baadhi ya viongozi katika sekta hiyo kuja na mabadiliko tofauti katika shughuli za utoaji huduma kulingana na matakwa yao bila ya kuzingatia weledi wa kazi hiyo.

Wamesema hali hiyo inasababisha kuwepo kwa malalamiko juu ya huduma zinazotolewa kwa jamii.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano mkuu wa chama hicho unaofanyika jijini Mwanza na kuiomba serikali kuanzisha utaratibu wa mafunzo ya afya kwa viongozi hao katika ngazi za mikoa, halmashauri pamoja na wilaya kwa lengo la kuwapa uelewa juu ya kanuni na taratibu za sekta hiyo.

"Tunaishauri serikali iweke bajeti ya kuwapa semina viongozi wanaoteuliwa katika nafasi mbalimbali lengo likiwa ni kuondoa mkanganyiko wa mara kwa mara katika sekta muhimu katika maisha ya wananchi kwani kwa kufanya hivyo kutaleta tija kubwa kwa taifa letu,"alisema.

Mawala alisema chama hicho, kina wanachama zaidi ya 800 ambao ni makatibu wa afya kutoka mikoa yote ya Tanzania, kinakabiliwa na tatizo la kutokuwepo kwa baraza ambalo lingesaidia kutatua matatizo ya kitaaluma kwa watumishi wasio na weledi.

Naye Katibu Mstaafu wa taaluma hiyo, Dk. Anna Nswila, alisema chanzo cha malalamiko ya wananchi juu ya upatikanaji wa huduma ya afya yanatokana na wanataaluma wenyewe kushindwa kufuata weledi sambamba na ukiukwaji wa maadili ya kazi.

"Suala la kuwapa ajira na madaraka makubwa katika taaluma ya afya watu wanaotoka vyuoni ambao hawana uelewa wa kazi kunaharibu utendaji na utoaji wa huduma za afya," alisema na kuongeza:

"Kunasababisha malalamiko yanakuwa mengi kwa sababu hawana ujuzi na wamebakia kubebwa tu, hivyo katibu mkuu anatakiwa kuchambua nani anafaa maana unaweza kuwa na watu wengi lakini utendaji kazi mbovu".

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Seif Shekarage, alisema malalamiko yamekuwa mengi kutokana na watoa huduma kushindwa kutofautisha utaalamu wa sasa na wazamani.

Hivyo aliwataka makatibu hao kufanya uchunguzi kwenye maeneo yao ya kazi kwa lengo la kuainisha sehemu yenye shida zinazoweza kutatulika wazitatue haraka ambazo ni ngumu kwao waziwasilishe kwake.



Meneja wa Biashara wa Kampuni ya Mkulima Hub, Fakili Shaibu, akitoa elimu ya kutumia mfumo mpya wa kidijitali wa upimaji wa zao la pamba kwa baadhi ya wakulima na viongozi wa AMCOS, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga juzi, ambao unatarajia kutumika msimu huu kupima zao hilo. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Sungusungu wapewa jukumu vita ndoa za utotoni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limewapatia majukumu Jeshi la Jadi 'sungusungu' kuhakikisha linawafichukua wazazi na walezi ambao wamekuwa wakiwaozesha wanafunzi wenye umri mdogo.

Sungusungu walipewa jukumu hilo juzi na Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na wananchi katika kufichukua vitendo vya uhalifu uliofanyika Kata ya Majengo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Alisema, ushirikishwaji wa Jeshi la Jadi katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia umeanza katika wilaya zote za mkoa huo ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi kutojichukulia sheria mkononi.

Aidha Magoma aliwataka wafanyabiashara pamoja na kampuni za ulinzi kuajiri walinzi waliopitia mafunzo na kuacha utaratibu wa kuajiri wazee ambao mara nyingi wanatumia muda wa lindo kusinzia.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha kuuawa na kuibiwa kwa mali zao kirahisi, hivyo kuahidi kuziwajibisha kampuni zitakazoajiri wazee.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliyataja matukio yaliyokithiri wilayani humo kuwa ni pamoja na mauaji ya wivu wa mapenzi, ubakaji, ulawiti, ndoa za utotoni pamoja na matukio ya ndoa ya jinsia moja. Alisema kila mtu katika eneo lake anatakiwa kuwa balozi wa kupambana na vitendo hivyo ili kuvikomesha visiendelee kuwepo.

Hamis Juma ni mkazi wa Majengo alisema awali walikuwa waoga kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi wakiogopa pale watakapojulikana wanatengwa na watu wanaowazunguka.

Alisema kutokana na hamasa waliyopewa imewaondolea hofu hiyo na wako tayari kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kufichua vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ndoa za utotoni kwa wanafunzi.



Ukurasa 12

Mkurugenzi TARI: Makubwa bajeti kilimo Awamu Sita, tumefanyia mapinduzi mbegu, teknolojia hadi maabara




Ukurasa 13

Matatizo yasitumike kama fursa ya utajiri

BUFE
IJUMAA MEI 19, 2023
Nipashe




Ukurasa 14

**Darasa mazingira na biashara lilivyoinua wanawake wafugaji kijasiriamali, kuimiliki**

HIFADHI YA KATAVI

# Samia na Royal Tour, wageuka nyenzo ya ushindi soko watalii

## • Rasmi, aliyoyatamka kwenye uzinduzi...

**Na Mwandishi Wetu**



Viboko, vivutio vinavyokaribisha mgeni, wakiwa katika mabwawa ya maji Hifadhi ya Taifa ya Katavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

NI siku chache tu filamu ya kitalii Royal Tour yenye mhusika mkuu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuzinduliwa nchini Marekani, siku chache baadaye, msomi Dk. Ahmad Sovu, akaingia kwenye mtandao akifafanua manufaa yake.

Dk. Sovu anaorodhesha manufaa hayo kwa msemo "safari moja huanzisha nyingine au mkaa bure si sawa na mtembea bure..."

Akaendelea na simulizi namna Aprili mwaka jana Rais alivyorejea na kuzindua filamu hiyo jijini Arusha, shabaha kubwa ni kuitangazia dunia utajiri wa Tanzania.

Hapo Rais Samia akasisitiza kwa kauli: "Tujitayarishe kupokea wageni kwa kuepusha kutukuwapa usumbufu."

Kimsingi, ndicho sasa kinashuhudiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi, ambacho sasa kuna mapinduzo ya watalii wageni, takwimu zikiongezeka kila kukicha na asilimia kubwa, ni wanaotoka Marekani, nchi ambayo filamu hiyo ilizinduiliwa, kablaya kuzinduliwa nchini mkoani Arusha.

### IDADI YA WATALII

Mhifadhi Daraja la Pili, Hifadhi ya Katavi, Beatrice Msuya, anainisha tamkwimu, watalii wa nje waliotembelea hifadhi hiyo katika kipindi cha miaka mitano, imeongezeka kutoka 266 kwa mwaka 2018/2019 hadi watalii 815 wa sasa.

Kwa mujibu wa mhifadhi hiyo, idadi hiyo 815 ni watalii waliowatembelea kati ya Januari 2023 na sasa, wengi wanatoka Marekani, ambako sinema ya Royal Tour ilizunduliwa.

Pia, Mhifadhi Beatrice anasema, watalii wa ndani katika kipindi cha miaka mitano imeongezeka kutoka 290 mwaka 2018/2019 hadi 2,438 mwaka huu pekee.

### YALIYOMO HIFADHINI

Inaelezwa, mtalii anapokea makundi makubwa ya wanyama, wakiwamo viboko, nyati, simba, hata twiga, huku kukipambwa na mandhari tulivu na tambarare yenye nyasi fupi, mabwawa, misitu ya miombo, safu za milima, maziwa na mito inayotiririsha maji.

Ni hifadhi iliyoanzishwa mwaka 1974, ikiwa na ukubwa kilomita za mraba 2,253 na ikaongezwa asilimia 98, mara baada kuunganishwa Pori la Akiba la Rukwa, ikiwa na ukubwa kilomita za mraba 4,471.

Panatajwa kuwa mahali kunakopatikana mti ya mkwaju wenye utamaduni wa kabila Wabende na Wapimbwe, wanaoituimia kwa shughuli za matambiko kwa miaka mingi, ikiaminika inatunza mzimu maarufu kwa jina la Katabi.

Kaimu Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Manendo Peter Maziku, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Katavi, anasema pana utajiri wa wanyama wengi, mvua za kutosha, mito yenye maji mengi na maziwa mawili; Katavi na Chada inayofikika na kirahisi kwa kutumia usafiri wa barabara, ndege na treni.

Hapo Maziku, anataja hisani na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi, kupitia sinema ya Royal Tour, hata imeleta mapinduzi ya wateja wataalii wanaotembelea hifadhi hiyo.

Maziku anasema, wameboresha miundombinu ya hifadhi ikiwamo barabara, eneo la kupumzikia wageni, mabanda ya wageni, pia vyoo kwa wageni.

### SIRI YA MAFANIKIO

Mhifadhi Beatrice anataja, pia kuimarishwa doria za ndege na magari hifadhini kumaliza ujangili na uvamizi wa mifugo, huku wakitoa elimu kwa wananchi nje ya hifadhi wanaotumia maji Mto Katuma, kuacha kuyachepushia mashambani mwao.

Lingine anataja ni kuundwa vikundi vya ulinzi shirikishi katika vijiji vinavyozunguka hifadhi, vikishirikiana na askari wa hifadhi.

Vilevile anasema matukuo ya kuvamiwa mifugo, udhibitio wake umeonyesha mafanikio.

Beatrice anadems, Hifadhi Katavi, anataja mikakati yao kukuza utalii, inajumuisha kuitangaza kupitia vyombo vya habari ndani na nje ya nchi, vilevile kwenye maonyesho ya kimataifa.

Anadems, tayari Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kanda ya Kusini, inayojumuisha hifadhi Katavi, Ruaha na Kitulo, wanashiriki maonyesho hayo kujitangaza.

### UJIRANI MWEMA

Mhifadhi Mwandamizi, Francis Kone, anasema Hifadhi ya Katavi, inatoa misaada kwa ajili ya miradi mbalimbali jirani katika miaka mitano iliyopita.

Anadems ni fedha kutoka TANAPA kwa ajili ya kuchimba visima vya maji vijiji vya Sitalike, Igongwe na Matandarari, vyote kila kimoja kikipatiwa Sh. milioni16 (jumla Sh. milioni 48), katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mingine ni jengo la Kituo cha Afya Mwamapuli (Sh. milioni 112), kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kisima cha maji kijiji cha Lukima kata ya Majimoto (sh 17.5 milioni),

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

# Mkurugenzi TARI: Makubwa bajeti kilimo Awamu Sita, tumefanyia mapinduzi mbegu, teknolojia hadi maabara

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

UTAFITI wa kilimo imo katika orodha muhimu ya kusaidia kuharakisha mabadiliko ya kitaalamu ya sekta ya uzalishaji wa mazao nchini, kupitia kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji na tija.

Ndani ya tafsiri hiyo, serikali ya awamu ya sita iliyoko madarakani imeipa kipaumbele, ikiiongezea mgao wa bajeti sekta hiyo, kutoka Sh. bilioni 294 za mwaka mmoja kabla, hadi Sh. bilioni 751 iliyoidhinishwa siku chache zilizopita katika mwaka wa fedha 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 158.

Takwimu zinaonyesha umuhimu wa sekta ya kilimo ikiajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, pia inachangia asilimia 27 kwenye Pato la Taifa (GDP), asilimia 60 ya malighafi na asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Hata hivyo, inapiga hatua za maendeleo ya uwezeshwaji kuneemesha uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula, sekta hiyo nchini bado inakabiliwa na vikwazo vinavyodhoofisha maendeleo yake.

Katika orodha hiyo, inatajwa kuwapo ufinyu wa fedha za kuwezesha taasisi na wataalamu wa kilimo kufanya

utafiti wa kina, hivyo serikali imekuwa ikifanya mikakati ya kuongeza ufanisi wa sekta hiyo nchini.

Vilevile ndani ya kilimo kunatajwa kuwapo bajeti rafiki, inayoshuhudia fedha za kibajeti za utafiti, zikiongezeka kutoka Sh bilioni 11.63 hadi Sh. bilioni 40.73, hatua inayotajwa kuiwezesha, ndai ya miaka hiyo miwili ya awamu ya sita, chini ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan.



Rais Dk, Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Kilimo Hussein Bashe (katikati) na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI),akikagua mbegu za mazao. **PICHA: MTANDAO**

Hatua hiyo inatajwa ni muhimu, hata Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, anafafanua akisema imeiwezesha taasisi yake kufanya kazi yenye tija, akitaja mapinduzi ya tafiti za mbegu za mazao, ndani ya miaka miwili hadi sasa.

Dk. Geoffrey Mkamilo, anafafanua: "Dhima ya TARI ni kugundua na kuhimiza matumizi ya teknolojia mbalimbali za kilimo, ili kuongeza tija, uhakika wa chakula na lishe, kuwa na kilimo endelevu na chenye mchango chanya katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kushirikiana na wadau wa kilimo wa kitaifa na kimataifa kwa ujumla".

Kwa mujibu wa Dk. Mkamilo, katika miaka miwili hadi sasa,TARI imeshatafiti na kugundua aina 25 ya mbegu bora za mazao, zilizoidhinishwa kutumiwa na wakulima, akizitaja kuwa mbegu bora zilizoidhinishwa na Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI).

Anaorodhesha kwa ufafanuzi wa idadi na aina zake kwenye mabano ifuatavyo: Mtama (mbili), migomba (nne), viazi vitamu (mbili), miwa (sita),maharagwe (sita), ngano (mbili), choroko (mbili) na aina moja ya mpunga.

Dk. Mkamilo anaeleza kuwa aina hizo ni zinazostahimili ukame na magonjwa, zikiwa na uwezo mkubwa wa kutoa mazao mengi, na anamshukuru Rais kuweka mkazo katika kuisaidia taasisi yao kupanua wigo wa kufanya tafiti za mbegu nchini.

"Kwa mfano, mbegu za ngano tulizozivumbua, zina asilimia 38.9 ya gruneti, protini inayohitajika sana katika viwanda vya uzalishaji, zina uwezo wa kuzalisha kati ya tani nne hadi 4.6 kwa hekta," anaeleza.

Pia, anaongeza kwa mara ya kwanza, TARI imefanikiwa kugundua na kuzalisha mbegu za miwa zenye uwezo wa kuendana na hali ya mvua, hatua muhimu inayotarajiwa kuwasaidia wakulima wadogo kupunguza gharama za uzalishaji, ikilinganishwa na mbegu za awali zinazotegemea ardhi ya maji na umwagiliaji kwa asilimia 100.

"Tafiti zetu zimefanikiwa kugundua nafasi mpya ya kupanda pamba ambayo ni sentimita 60 kwa sentimita 30, hatua muhimu ambayo imechochea ongezeko la mavuno kutoka wastani wa kilo 710 hadi 1,422 kwa ekari," anasema Dk Mkamilo.

Bosi huyo mkuu wa TARI, anasema katika juhudi za kuongeza tija ya uzalishaji pamba nchini, wametafiti na kugundua zana rahisi ya kupanda pamba, yenye uwezo wa kupanda ekari moja kwa saa moja hadi saa tatu,badala ya saa 11 kwa kutumia jembe la mkono.

"Ugunduzi wa mashine hii kwa kiasi kikubwa umepunguza upoteaji wa mbegu kutoka asilimia 15 hadi tano," anafafanua, ikiwa ni zao la mageuzi ya taasisi anayotumikia katika miaka miwili iliyoko ya uongozi kitaifa ulioko madarakani, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

### TEKNOLOJIA MPYA

Vilevile anataja TARI imegundua teknolojia rahisi na rafiki za kuhifadhi nyanya na juisi za miwa kwa zaidi ya miezi miwili, pasipo kupoteza ubora wake, kwa kutumia

viambata asilia tofauti na njia za kawaida, zenye uwezo wa kuhifadhi kwa siku mbili pekee.

"Taasisi imeendelea kutunza vinasaba vipatavyo 33,332 vya mazao mbalimbali ikiwamo mpunga (729), mtama (416), uwele (105), ulezi (3), alizeti (39), zabibu (26), migomba (128), maharagwe (10), muhogo (20), korosho (30,000), pamba (328), mahindi (250), viazi vitamu (6), miwa (107), minazi (7), michikichi (3), mkonge (60), na kakao 17, kwa lengo la kuzuia upotevu wa vizazi hivyo na kuwa na utafiti endelevu," anaeleza.

Pia, katika kipindi hicho cha miaka miwili, Dk. Mkamilo anasema TARI imeongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 481,23 mwaka wa fedha 2020/21, hadi kufikia tani 1,225.872 mwaka 2021/2022.

Hapo anaainisha mkakati wa kuzalisha miche, vikonyo na pingili ulioongezeka kutoka 7,998, 784 kwa mwaka 2021/22 hadi 19,822,349 kwa mwaka 2023, yakihusisha mazao ya parachichi,michikichi, mihogo, miwa, viazi mviringo, korosho, matunda na viungo.

" Kwa upande wa usambazaji wa teknolojia bora za kilimo, tumefanikiwa kuzindua vituo mahiri vinne vya kusambaza teknolojia kwa wakulima, ikijumuisha kituo cha Nyakabindi (Simiyu), Nzuguni (Dodoma), Fatma

Mwasa ( Tabora) pamoja na kituo cha Mwalimu Julius Nyerere Morogoro," anaeleza.

### UHAKIKI MABADILIKO

Katika kuhakikisha matokeo ya utafiti yanaleta mabadiliko chanya kwenye sekta kilimo nchini, Dk. Mkamilo anasema, taasisi yao imepeleka matokeo ya utafiti mbalimbali kwa wadau 5,497,547 wakiwamo wakulima na maofisa ugani.

"Njia zilizotumika kusambaza teknolojia hizo ni pamoja na maonyesho ya wakulima, siku za wakulima, maonyesho ya kilimo biashara, mafunzo wezeshi, majukwaa bunifu na mashamba darasa," anaeleza.

Pia, moja na njia hizo, amesema pia wamekuwa wakitumia vyombo mbalimbali vya habari, ikiwemo redio, magazeti, televisheni na mitandao ya kijamii katika kuwaelimisha wakulima juu ya matumizi sahihi ya teknolojia hizo zinazolenga kuongeza uzalishaji na tija katika uzalishaji mazao ya kilimo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa TARI, taasisi inaendelea kuongeza uzalishaji na upatikanaji mbegu bora nchini, wakiboresha mahitaji ya utafiti na uzalishaji na kwa miaka miwili hadi sasa, ameshaandaa ujenzi wa miundombinu ya kumwagilia hekta 854 zinazopatikana kwenye vituo 16 vya utafiti nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Mkamilo, kukamilika ujenzi wa miundombinu hiyo utawezesha uzalishaji wa mbegu na majaribio ya utafiti kufanyika mwaka mzima.

"Tupo pia katika hatua nzuri ya ujenzi wa maghala matano ya kuhifadhi mbegu yenye vyumba vya ubaridi katika vituo vya TARI Naliendele, TARI Tumbi, TARI Hombolo, TARI Selian na TARI Dakawa, mradi ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 10," Dk. Mkamilo anaeleza.

Pia, anasema TARI imeanza kukamilisha taratibu za kuwezesha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo iliyopo katika kituo chake cha Mlingano Tanga, akifafanua:

"Kwa sasa hatua iliyofikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na vitendanishi vya maabara na kufanya tathmini ya uwezo na ubora wa maabara hiyo, mchakato ambao umefikia asilimia 40,"

Anasema kuna ukarabati wa maabara nyinginezo katika vituo vya Tengeru, Mikocheni na Mlinganom, mahsusi kwa uzalishaji wa miche kwa njia ya chupa, utambuzi wa magonjwa na wadudu, kupima mbegu na kutathmini afya ya udongo.

### TARI ILIKOTOKA

TARI, iliyoanzishwa kisheria mwaka 2016, inatekeleza majukumu yake kupitia mtandao wa vituo 17 vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini.

Vituo hivyo vya TARI ni Naliendele (Mtwara), Uyole (Mbeya), Ukiligulu (Mwanza), Kihinga (Kigoma), Mlingano (Tanga), Kibaha (Pwani), Mikocheni (Dar es Salaam), Maruku (Kagera), Kifyulilo (Iringa), Ilonga (Ifakara), Dakawa (Morogoro), Selian (Tengeru), Tumbi (Tabora) pia Makutupora na Hombolo (Dodoma).

# SAMIA NA ROYAL TOUR, WAGEUKA NYENZO YA USHINDI SOKO WATALII

**INATOKA UK.11**

mwaka 2018/2019.

Kuna ujenzi wa vyoo vya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Usevya, sambamba na Sh. milioni 33 za kujenga madarasa; huku ofisi ya walimu Shule ya Msingi Kasegenyama, ina Sh milioni 45 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Vilevile, ujenzi wa bweni la wasichana Shule Sekondari Sitalike, uliopokea Sh milioni75 kwa mwaka wa fedha mwaka 2020/2021.

Aidha, anataja hifadhi imeendelea kuhamasisha watu wanaoishi jirani,watembelew hifadhi ili kuwaongezea uelewa wa yaliyomo.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Sekondari ya Sitalike,wanufaika wa msaada wa hifadhi, Silivester Lameck, anaishukuru TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Katavi, kwa kuwajengea bweni litawaondolea tatizo la mabinti kutembea umbali mrefu, pia wakiepuka vitendo vya unyanyasaji kijinsia wakiwa shule.

"Tunaishukuru sana TANAPA, wametusaidia sana, kwani bweni hili lina uwezo wa kutumiwa na wasichana 80," anasema Mwalimu Lameck.

Mmiliki wa Hoteli ya River Side, Juma Kiambile, anasema jitihada za serikali kutangaza vivutio vya utalii, zimesaidia kuongeza utalii wa nje wanaotembelea, Hifadhi ya Katavi, ikilinganishwa na awalihuko nyuma.

Pia, anataja maboresho yaliyowezesha kuwapo barabara ya lami kutoka Mpanda hadi Tabora na Mpanda hadi Mbeya, pia usafiri wa ndege wa uhakika, treni na kufunguliwa na Bandari ya Karema, inayounganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kumefungua milango ya utalii hifadhini Katavi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Igongwe, Ephraim Mwambulu, anaishukuru Hifadhi ya Katavi kuanzisha utaratibu wa kufadhili makundi ya wakazi kando ya hifadhi, pia kupatembelea kuona vivutio vyake kila mwaka, ukiwa mpango wa kuboresha uhusiano na jamii.

Anasema amepata fursa hizo kila mara, licha ya akitoka kijiji jirani, lakini anakabaki hifadhini kwa hadhi ya utalii, inamfanya kushuhudia vingi, wakiwamo wanyama wakubwa; simba, chui, tembo na twiga na kuelezwa maisha na tabia zao.


Mfugaji kutoka kitogonji jirani, Kasongwa, anaishukuru Hifadhi ya Katavi kuwapatia elimu ya uhifadhi, hata sasa wanajua umuhimu wa hifadhi kwa nchi, sasa anatoa wito kwa wafugaji wenzake wanaoishi kando na hapo, kuacha kuharibu mazingira.

### CHANGAMOTO ZILIZOPO

Hata hivyo, Hifadhi ya Katavi inakabiliwa na matatizo, ikiwamo kukauka mto Katuma wakati wa ukame, unapita ndani ya hifadhi kumwaga maji Ziwa Rukwa, sababu kuu ni wakulima kuchepushia maji mashambani mwao, hali inayowaathiri wanyama.

Mhifadhi Maziku anataja lingine, ni adha ya ujangili wa wanyama, pia kugongwa na magari yanapita katika barabara tatu ndani ya hifadhi, ambazo ni; Sitalike-Kizi, Mpanda-Sitalike-Kibaoni na Majimoto-Inyonga-Sikonge.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Matatizo yasitumike kama fursa ya utajiri



**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**(kulangwasos@gmail.com)**

HURUMA ni hali impatayo mtu mwenye roho nzuri, pale aonapo mwenzake anapitia kipindi kigumu cha maisha na hatimaye kutamani amsaidie kuondokana na hali hiyo na hatimaye aishi kama wengine.

Ni kweli, kuwa binadamu hatufanani wala kulingana kimaisha, kutokana na hali ya kipato, lakini pia afya aliyonayo kila mmoja. Ndiyo sababu tofauti ya matajiri na masikini ni jambo lisiloepukika.

Kuna watu duniani ambao wameona watu wakiteseka kimaisha na kuamua kuwasaidia wao moja kwa moja au kupitia watu au taasisi zingine, huku wao wakiweka mazingira ya kukaribisha usaidizi huo.

Vituo vya habari hususan redio na televisheni, vimekuwa mstari wa mbele nchini kutengeneza mazingira ambamo watu wenye matatizo ambao mara zote ni wa hali ya chini kiuchumi husaidiwa.

Kuna vituo kadhaa vya redio ambavyo vimekuwa vikijikita katika hilo na kupata wasikilizaji wengi ambao hujitokeza kusaidia wenye matatizo kama hivyo, ingawa si rahisi kuyamaliza.

Upo mtindo wa vituo hivyo kuigana, pengine ni kutokana na kuwa vingi na kukosa umahiri wa kuandaa vipindi tofauti, hivyo kimoja kusubiri kingine kuja na wazo na mara moja nacho kuiga.

Ni sawa na mtaani, ambako mtu ataanzisha biashara ya vitumbua na mwingine akiona mwenziwe anapata wateja, naye atafungua biashara hiyo hiyo na kujikuta wakigombea wateja hao hao wachache.

Matokeo yake ni biashara kufa kwa kukosa wateja, au wafanyabiashara wenyewe kuoneana inda na wivu na kufanyiana hiyana na kusambaratishana. Hayo ndiyo huwa maisha ya mitaani.

Nimekuwa miongoni mwa wasikilizaji wa vipindi vya kusaidia wenye matatizo, ambapo waandaaji hualika kila mwenye tatizo kufika studio na kuhojiwa chanzo cha matatizo na nini anataka na kisha hutoa namba za simu ili kuomba msaada.

Kweli, kuna wasikilizaji ambao hupiga simu na kuahidi kutoa kitu kwa ajili ya mwombaji, na hatimaye hupewa lakini mara nyingi matatizo huwa hayamaliziki, kwani mengi huwa yanahusiana karibu sana na matatizo ya kiafya.

Kama ijulikanavyo, matatizo ya kiafya ni aghali kuyamaliza, kwa kuwa yanahitaji mchakato wa kuonana na daktari, vipimo na hatimaye tiba ambayo yawezekana isipatikane nchini, na mgonjwa kulazimika kupelekwa nje.

Ukipata fursa ya kusikiliza baadhi ya wenye matatizo, utatambua jinsi wanavyoishi maisha magumu sana kulingana na wanavyojieleza. Baadhi yao utawasikia wakilalamika kuwa na watoto na kuishi nao mitaani au kwenye mapagala.

Sababu za hali hiyo, utaambiwa ni ama kifo cha mzazi mmoja hususan wa kiume au kutelekezwa na mzazi huyo huyo na kumwacha mama na wanawe wakiishi katika mazingira hayo hatarishi.

Mwingine utamsikia akilalamika kuwa anapoishi ambako ni kwenye pagala, hana kitu chochote cha kula wala kulalia na wanawe wawili au watatu na hata nguo alizovaa ni hizo hizo hana zingine.

Lakini, jambo ambalo mimi pengine na wengine wanaofuatilia matatizo haya hushangaa, ni pale mwenye matatizo anapoombwa kutaja namba ya simu ili atumiwe msaada, anataja tena namba mbili au zaidi za simu akimaanisha ana simu zaidi ya moja.

Na huyo anakwambia analala kwenye pagala (jumba ambalo halijakamilika ujenzi). Unajiuliza katika pagala hilo, mtu huyu anachaji wapi simu yake/zake! Au mtu huyu ambaye hana pa kula, hana mavazi, hana pa kulala anawezaje kumiliki simu?

Wengine hutumia simu za watu wengine, je, unajiuliza, kuna uhakika gani wa usalama wa fedha hizo zinazotumwa kwa ajili ya msaada huo, hata kama atatumia simu ya kituo cha redio, kuna uhakika wa usalama wa mchango? Je, si mradi wa watu?

Maswali yanakuwa mengi na hasa tukirejea kwenye amri ya Serikali wakati fulani, dhidi ya ombaomba mitaani wakitumia watoto kuwasukuma kwenye vitimwendo na wengine kukaa kando mwa barabara na kutanguliza watoto!

Kama kuna ulazima huo wa kusaidia wanaoishi katika mazingira magumu, basi Serikali kupitia Wizara yenye dhamana, ijenge vituo vingi vitakavyolea watu wenye matatizo kama hayo wakiwamo watoto, na wananchi wenye uwezo wa kuchangia wakazipeleka huko.

Vinginevyo, matatizo ya watu yataendelea kutumika kama fursa kwa wengine, ili mradi tu wana miundominu ya kuwavuta na kuwatambulisha kwa jamii yenye wasamaria wema walio tayari kujitoa kusaidia. Alamsiki!

UCHUMI

# Darasa mazingira na biashara lilivyoinua wanawake wafugaji kijasiriamali, kumiliki




Baadhi ya wanachama wa kikundi cha vikoba Galilaya, Babati wakiwa kwenye mjumuiko wao, **PICHA: JENIFER GILLA.**

**Na Jenifer Gilla**

Ni saa 12.00 jioni, Happy Longei, Mkazi wa Kijiji cha Mswakini, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, amesimama kwenye mlango wa zizi la ng'ombe akishikilia vibuyu vitatu vya maziwa baada ya kumaliza kukamua, haamini kama kimoja ni mali yake isiyo na masharti, fikra zake zikirudi mwaka mmoja nyuma, sasa anaona mabadiliko makubwa.

Huyo ni mwanamke wa jamii ya wafugaji Wamasai, ambao ilikuwa ni mwiko kwao kumiliki mfugo, hata kutoa uamuzi juu ya maslahi binafsi, licha ya kazi ya kuihudumia aliyofanya, ikiwamo kupelekea mifugo malisho, kusafisha zizi na kukamua maziwa asubuhi na jioni.

Mali yake kubwa ilikuwa maziwa yanayokamuliwa asubuhi tu, tena yaliyobaki baada ya kutenga ya matumizi ya nyumbani. Maziwa ya jioni pamoja na faida ya kuuza ng'ombe ni mali ya baba, jambo ambalo ni kinyume na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000, inamyotaka mwanamke kushiriki katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii vizuri zaidi .

“Kama hiyo siku maziwa ya asubuhi hayakupatikana mengi sipati ya kupeleka mnadani kuuza, yakipatikana mengi ndio napata kama lita mbili naenda kuuza, pesa inatumika kununulia watoto mafuta na sabuni ya kutumia hapa nyumbani, kuna wakati nilikuwa nahisi unyonge lakini sasa umekwisha,” anasema Happy.

Unyonge wa mama huyo mwenye mume na watoto watatu, ukakoma mwaka jana baada ya kikundi chao cha vikoba kinachoitwa Galilaya, kutembelewa na taasisi binafsi ya Ujamaa Community Resource Team (UCRT), hata wakapewa elimu ya kujitambua, sasa imewanyanyua, wakiitegemea kiuchumi.

Kupitia taasisi hiyo Happy na wana kikundi wenzake 30 wamepata elimu ya kufuga kisasa, wakinenepesha mifugo, biashara na pesa za kutunisha mfuko wa kikundi hicho, ndipo akachukua mkopo Sh. 500,000 akanunua ngombe wawili sasa jike limezaa mapacha na linatoa lita nne ya maziwa kila siku, anamiliki bila kupimiwa na mumewe.

Kupitia biashara ya kuuza maziwa hayo, Happy ana uhakika wa kupata si chini ya Sh. 5000 kwa siku anazotumia kuhudumia watoto na kulipa marejesho ya mkopo kila wiki.

Pia, ameeshaongeza mifugo ya kuku ambao mara anapouza, inamsaidia kulipa deni, jambo analosema limemuongezea heshima kwa mumewe.

Upande wa pili, anakumbusha akiwa kama mama wa nyumbani akiwa na jukumu la kuingia msituni kukata miti kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, sehemu ya mkopo alinunua gesi kuondokana na uharibifu wa mazingira na kuchochea ongezeko la mabadiliko ya tabianchi, sasa anatumikia elimu aliyoipata kupitia UCRT.

Happy ni kati ya wanawake 90 walionufaika na mikopo, elimu ya kufuga kisasa, biashara na madhara ya kutumia kuni kiafya na kimazingira.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mawakini Violet Elias, ni jambo lililobadilisha maisha yao kiuchumi na kuwaondoa kwenye utumwa wa waume zao, sasa wanahamasisha mabadiliko katika jamii zao.

Mwingine ni Yasinta Tango, aliyenufaika na mkopo Sh. 700,000 akanunua mbuzi watatu, kuku sita na sehemu ya pesa akanunua gesi ya kupikia, baada ya kuona faida zake kiafya na kiuchumi, ikiwamo kutumia muda mdogo kupika, anapata muda zaidi wa biashara zake.

“Nilipouza kuku mwezi uliopita kiasi cha fedha nikaanzisha biashara ya kuuza maandazi jioni na faida yake zinanisaidia kuongezea fedha za kulipia deni ninalodaiwa vikoba,” anasema.

Mama huyo anasimulia alikotoka, ilikuwa vigumu kumhamisha mume wake kutoka kwenye dhana ya kutumia kuni, kuelekea kwenye gesi, akimhamisha kutoka imani kuwa gesi zinalipuka kila mara na kuwasababishia vifo.

Happy anataja pesa za mkopo zilimuwezesha kununua gesi na kuipeleka nyumbani na baada ya kutumia muda mrefu bila madhara mume wake akaridhika.

“ Baada ya kuipeleka ile gesi nyumbani kwa nguvu, mume wangu alikasirika na kuniambia watoto wake wakilipuka nitawalipa, lakini kwa kuwa tulielekezwa njia salama za kutumia gesi na ninazifuatilia vizuri, sasa ni miezi sita hakuna madhara yoyote yametokea hata mume wangu sasa anasaidia kubadilisha mtungi” anasimulia.

**MWENYEKITI NA HISTORIA**

Mweyekiti wa kikundi hicho, Suzana Leonard, anasema kikundi hicho kilianza mwaka 2018 kama Baraza la Haki la Uongozi wa Wanawake, kikiwa na wanachama 30 wa kutetea haki za watoto wa kike wanaonyanyasika kijinsia.

Anasema, walichanga kila mmoja Sh.5000 wakanunua mbuzi 24 wa kufuga, kwa lengo la kugawana pale wanapozaa, lakini mwaka 2021 mifugo tisa ilikufa, kutokana kukosa malisho bora, baada ya kuibuka ugonjwa wa UVIKO-19 uliolazimisha familia kukaa ndani na kupunguza misongamano.

“Kipindi cha uviko-19 kikoba kiliyumba, mpaka mwaka jana tulipotembelewa na UCRT na kutupa elimu ya biashara na Sh. milioni saba ambazo tumenunua viti 100 kwa ajili ya kukodisha na nyingine tumekopeshana kwa ajili ya miradi ya mtu mmoja mmoja, ambayo ndio imetuwezesha kununua gesi na kuondokana na matumizi ya kuni kupikia,” anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, malengo ya kikundi ni kuongeza viti idadi ifike 300, kununua turubai ya kukodisha na bajaji ya kupelekea viti kunakohitajika, ili kurahisisha huduma na kuwavutia wateja wengi, hata wapate faida nyingi.

Vilevile, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mawakini, Violet Elias, anasema tangu kutembelewa na UCRT wamehamasisha wanawake wengi kujiunga na vikoba ili kupata mikopo, kuachana na matumizi ya kuni kutoka kikundi kimoja na sasa vipo vitatu vyenye jumla ya wanachama 90, vipo chini ya Baraza la Haki la Wanawake na Uhifadhi Mazingira.

Anasema, mikopo hiyo pia imewaondoa wanawake kutoka kuwa wategemezi wa chanzo kimoja cha biashara ambapo walikuwa wakitegemea kuuza maziwa na baada ya mifugo kufa na biashara zikafa lakini sasa wanafanya biashara nyingine ikiwamo kuuza maandazi, migahawa na kufuga kuku.

“Katika jamii ya kifugaji japo kuwa mwanamke anafanya kazi ngumu ya kulisha mifugo, lakini mali yake pale ni maziwa tu na anaruhusiwa kuuza yale yaliyobaki baada ya kutoa ya kutumia nyumbani.

“Ng'ombe ni mali ya baba yeye ndio anauza na hela ni ya kwake, kwa hiyo kadiri mifugo inavyopungua mama anaathirika zaidi, sasa tunashukuru tuna uwezo wa kununua mifugo yetu wenyewe na kufanya biashara nyingine,” anasema.

Meneja Mradi kutoka UCRT, Fred Loure, anasema mradi wa taasisi USAID - Tuhifadhi Mazingira, waliwafikia wanawake hao mwaka jana na kuwapa elimu biashara kupitia vikundi vya vikoba, lengo ni kuwashawishi kuachana na ukataji miti, wahamie kutunza maliasili, mazingira na wanyamapori.

“Moja ya elimu tuliyowapa ni ile ya kufunga maeneo ya malisho, tumewaelekeza kipindi kama cha sasa ambacho majani ya malisho yapo mengi, wafunge mapori yaliyotengwa kulisha mifugo ili yachipue, halafu watayafungua baada ya miezi mitatu kunakuwa na ukame, ili kuepukana na adha ya uhaba wa malisho, na hii imesaidia sana,” anasema.

Anasema mpaka sasa wamevifikia vijiji 127 katika wilaya 10 wakizilenga jamii za wafugaji, waokota matunda na warina asali, ikiwa na lengo la kumwezesha mwanamke kiuchumi kupitia vikoba, kuwajengea uwezo wanajamii wanufaike, wakitoa ufadhili kwa vijana kusoma vyuo na umiliki wa ardhi.

Kwa mujibu wa Shirika la Fedha Duniani (IMF), uwezo wa wanawake kumiliki fedha ni mdogo duniani, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni asilimia 37 tu ya wanawake wana akaunti za benki, ikilinganishwa na asilimia 48 ya wanaume, pengo likaongezeka katika miaka kadhaa iliyopita.

Ili kuondokana na adha hiyo na kukuza uchumi wa nchi, shirika hilo linaelekeza kubadilisha sera na kanuni ili ziwe rafiki kwa mwanamke.








Mkuu wa huduma za benki kidijitali wa Benki ya Azania, Vinesh Davda (wa pili kulia) na Meneja Taifa Biashara wa Kampuni ya Selcom, Geofrey Mwakamyanda (wa pili kushoto), wakizindua ushirikiano baina ya benki na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana, wenye lengo la kuboresha huduma za fedha kidijitali. Wengine ni Meneja Masoko wa benki hiyo, Allan Msalilwa (kulia) na Meneja Uhusiano wa Taasisi za Serikali wa Benki ya Azania, Angela Odhiambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC atoa siku 30 kukamilika ujenzi wa miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza watendaji wa halmashauri kusimamia ujenzi wa miradi inayoendelea kujengwa mkoani hapa na kuhakikisha inakamilika ifikapo Juni 20, mwaka huu.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kyala ambako alizindua mradi wa umeme uliotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) baada ya kuhitimisha ziara yake ya siku mbili kukagua miradi 30 ya maendeleo i kiwamo ya ujenzi wa shule mpya za msingi, madarasa, hosteli na zahanati.

Serukamba alisema hataki kuona fedha zilizoletwa katika Mkoa wa Singida kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zinarudi serikalini baada ya mwaka wa fedha kumalizika.

"Ifikapo Juni 30 serikali huwa inachukua fedha ambazo hazijatumika, sisi wakuu wa mikoa tunayo maelekezo mahsusi kutoka kwa Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tunahakikisha fedha hizi hazirudi maana yake tuhakikishe miradi hii inatekelezwa," alisema.

Serukamba alisema katika ziara yake wilayani Iramba amejifunza upande wa halmashauri na serikali watendaji wanatakiwa kuisimamia kwa karibu miradi inayotekelezwa badala ya kuwaachia walimu na wananchi waisimamie. "Kwenye 'project management' lazima muwe na 'culture' ya kusimamia miradi hii kwani Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo hivyo itakuwa jambo la ajabu tuliposimamia tukaacha isikamilike kwa wakati," alisema.

Aidha, Serukamba aliwahimiza wananchi kutunza miundombinu ya umeme na kulipa ankala kila mwezi ili kuiwezesha REA pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ziendelee kutoa huduma bora na za uhakika kwa wananchi.

Katika miradi 12 aliyoitembelea leo Mkuu wa Mkoa hakuridhishwa na kasi ya ujenzi shule mpya za msingi za Kibululu na Nselembwe na kuwaagiza walimu wakuu wa shule hizo wanapobaini mafundi ndiyo kikwazo wasisite kuwaondoa na kuweka wengine.

Aliwataka madiwani, viongozi wa vijiji na kata kuwahamasisha wananchi waweze kushiriki katika ujenzi wa miradi hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Gunna Maziku, alimhakikishia Serukamba kwamba yeye na viongozi wenzake watahakikisha wanaisimamia miradi hiyo na kukamilika ifikapo Juni 20, mwaka huu kama alivyotoa maelekezo.

# TMDA yatoa maagizo kwa wamiliki maduka ya dawa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba(TMDA), Kanda ya Kati imewataka wamiliki wa maduka ya dawa kuhakikisha wanaondosha dawa na vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi kwa mujibu wa sheria. Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa, aliyasema hayo alipokuwa akikabidhi dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.milioni 15.5 kwa Mkuu wa Gereza Msaidizi Msalato Dodoma. Alisema kuwa wakaguzi wa mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wakaguzi kutoka halmashauri za Dodoma itahakikisha inadhibiti kwa kukamata dawa na kuziondosha katika soko. "TMDA iliondosha katika soko dawa na vifaa tiba ambavyo vinafaa kwa matumizi lakini kwa mujibu wa sheria ya dawa na vifaa tiba hivyo havikupaswa kuuzwa au kutumika katika maeneo husika."

"Hivyo ukaguzi huo ulisababisha kuondosha katika soko dawa na vifaa hivyo vyenye thamani ya shilingi milioni 15.5 ambavyo bado ni bora na salama kwa matumizi kama ilivyoainishwa,"alisema.

Naye Mkuu wa Gereza Msaidizi na Mganga wa Zahanati ya Gereza la Msalato, SP Dk. Abusalum Mpamba, alisema kuwa msaada wa dawa uliotolewa na mamlaka hiyo utaenda kusaidia kwa kuwafikia walengwa na kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya.

# Wazazi wanaoficha watoto kutokwenda shule kushtakiwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UONGOZI wa Jiji la Dodoma umekemea tabia ya wazazi wasioandikisha watoto shule kwa kisingizio kwamba hawataki, huku ukiahidi kuwachukulia hatua kali wote watakao bainika kufanya hivyo.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, wakati akikabidhi sare za shule kwa watoto wanaotoka katika familia zisizo na kipato.

Wanafunzi 120 wa Shule ya Msingi Chigongwe, Buigiri na Msembeta za jijini Dodoma walishonewa sare za shule na Diwani wa Viti Maalum Manispaa ya Kinondoni, Grace Mwachala baada kuombwa na Meya Prof. Mwamfupe.

Prof. Mwamfupe alisema utamaduni wa kutoandikisha shule watoto wa darasa la kwanza umeota mizizi maeneo mengi ya Mkoa wa Dodoma hivyo wameamua kutafuta dawa ya tatizo hilo.

Alisema tabia hiyo haitapata nafasi katika kipindi cha uongozi wake kwani bila kuangalia uwezo wa kiuchumi wa familia anayotoka ni lazima mtoto apate elimu.

"Tatizo la uandikishaji kwa watoto wa darasa la kwanza bado linatusumbua, naagiza kuwa wazazi wasijifiche kwenye kivuli eti watoto hawataki kwenda shule, siyo sawa kabisa,"alisema Mwamfupe.

Hata hivyo aliiomba jamii ya wasomi kutoka vijijini ambao wamepata nafasi wakumbuke shule walizosoma ili washirikiane na kamati za shule kupeleka elimu kwa wazazi.

Diwani Mwachala alisema nguo alizowapa watoto hazikutoka mfukoni mwake bali alisikia kilio cha viongozi wa Jiji ndipo akakutanisha marafiki zake wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwasaidia.

Alisema baadhi ya maeneo aliyotembelea amejionea hali ngumu kwa baadhi ya familia ambapo zimemwachia deni namna atakavyowasaidia lakini akaomba watu wenye uwezo kujitokeza kuwapa faraja wahitaji kwani kufanya hivyo ni kujenga taifa la kesho.

"Binafsi sijajaliwa mali, lakini huruma yangu imenisukuma kufanya hivyo, nimetoa kwa wanafunzi kwa shule hizi tatu, nimetoa kwa kundi la watu wasioona ila nahisi kuwa na deni la kutoa zaidi na niahidi kuwa nitarudi tena baada ya kuchakalika huko na huko," alisema Mwachala.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Msembeta, Juma Mlawa, alisema shuleni kwake anaishi na watoto wanaotoka kwenye familia za kipato duni, wengi hawana uwezo wa kushona sare.





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akizungumza na Balozi wa Msumbiji nchini, Ricaldo Mtumbwide, alipomtembelea ofisini kwake jana, kwa ajili ya kujadili fursa mbalimbali za uwekezaji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbarali waipinga ripoti ya Waziri Mchengerwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kijiji cha Mwanavala kilichoko Kata ya Imalilo-Songwe wilayani Mbarali mkoani Mbeya wamepinga vikali ripoti iliyowasilishwa bungeni na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohammed Mchengerwa iliyokuwa inaeleza namna walivyonyanyaswa.

Waziri Mchengerwa alitoa ripoti bungeni kuwa hakuna mwananchi aliyepigwa wala kudhalilishwa na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya kama ilivyoelezwa na Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega.

Mbunge huyo aliibua hoja bungeni ya wananchi wa jimbo lake kunyanyaswa kwa kupigwa na askari, kuunguzwa na panga na kuporwa mifugo na akawaomba wabunge wenzake kumuunga mkono ili mjadala wa bajeti usitishwe na wajadili jambo hilo kwa dharura.

Hata hivyo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwaomba wabunge wasimuunge mkono Mtega na badala yake akamwagiza Waziri Mchengerwa kufuatilia jambo hilo na kumpelekea taarifa ya kinachoendelea katika eneo lililokuwa limetajwa.

Baada ya agizo hilo la Waziri Mkuu, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilifanya ziara katika Kijiji cha Mwanavala na kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho ambapo Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati hiyo aliagiza askari waliofanya ukatili kwa wananchi wakamatwe na kushtakiwa.

Siku moja baadaye Waziri Mchengerwa pamoja na baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Mbeya walifika katika Kijiji cha Mwanavala na kuzungumza na wananchi kuhusu kilichokuwa kimetokea na akamwagiza Katibu Mkuu wa Wizara yake kuwachukulia hatua za maofisa waliokuwa wameratibu operesheni hiyo.

Mbali na agizo hilo pia aliwakabidhi Sh. 5,000,000 waathirika wa tukio hilo la kudhalilishwa kama kifuta machozi.

Siku moja baada ya ziara hiyo, Waziri Mchengerwa aliwasilisha bungeni taarifa ya tukio hilo ambapo alisema hakuna mwananchi aliyedhalilishwa wala hakuna mifugo iliyopigwa risasi.

Taarifa ya Waziri imewakera wananchi wa kijiji hicho cha Mwanavala ambao wanadai kuwa imepotosha ukweli na inalenga kuwaumiza kwa maelezo kuwa matukio hayo yalitokea.

Mmoja wa wananchi hao, Golyama Chimya, alisema wakati anachunga mifugo pamoja na wenzake waliona ndege ya TANAPA ikiwa inashuka karibu na eneo walipokuwa wakaamua kukimbia ili kujiokoa wao pamoja na mifugo yao.

Alisema wenzake walikimbia na kufanikiwa kuokoa mifugo lakini yeye wakati anakimbia walishuka askari wawili kutoka kwenye ndege wakamkamata na kuanza kumpiga maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Alisema walimvua nguo wakaenda kuchukua panga kwenye ndege wakawa wanalipasha kwenye moto na kumpiga nalo mgongoni akiwa hajavaa nguo jambo ambalo lilimsababishia vidonda vikubwa.

“Walipotoka hapo walikwenda kwenye boma wakakusanya nguo zangu zote pamoja na vyombo wakachoma, lakini walipiga risasi mbwa watatu waliokuwapo pale kwenye boma na mbuzi watatu, nilikuwa nashindwa kutembea kwa sababu walinipiga sana maeneo ya kwenye unyao na walinichoma kwenye mapaja,” alisema Chimya.

Naye Mage Ntalamila alisema walimkuta kwenye eneo ambalo ni la makazi ya wananchi akiwa anatafuta ng’ombe wake ambaye alikuwa amepotea na wakaanza kumfukuzia kama wanataka kumgonga akaamua kulala.

Alisema walipomkamata walimvua nguo mbele ya wanawake ambao nao walikuwa wamekamatwa wakaanza kumpiga na panga la moto maeneo mbalimbali ya mwili huku wakiwa wamebana kwenye mti.

Alisema baada ya kumpiga walimwambia akimbie huku akiwa uchi jambo ambalo alisema lilikuwa la kumdhalilisha na hivyo akaiomba serikali kufuatilia upya jambo hilo.

Ana Satulo ambaye ni miongoni mwa wanawake waliokumbwa na tatizo hilo alisema alikuwa na watoto wake wa kike walikuwa wanachuma mboga aina ya mlenda wakaona ndege inashuka karibu na walipokuwa.

Alisema waliamua kulala kwenye kichaka ili isiwagonge lakini askari walishuka na kuwakamata wakawaambia wachuchumae na walipochuchumaa waliambiwa walale chini na wavue nguo zote.

Alisema waliokolewa na rubani wa ndege hiyo ambaye alikuwa mwanamke kwa kuwataka askari hao wawaache wasivue nguo na badala yake waondoke katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wafugaji wa Kijiji cha Mwanavala, Keyaa Sindole, alisema Waziri wa Maliasili na Utalii alipotosha taarifa ya tukio hilo kwa maelezo kuwa watu waliopigwa na kudhalilishwa wapo na mpaka sasa wanaugulia vidonda.

## Balozi wa Msumbiji afanya ziara mkoani Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BALOZI wa Msumbiji nchini, Ricaldo Mtumbwide, amefanya ziara mkoani Mbeya kwa lengo la kuangalia fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo nchi hizo mbili zinaweza kushirikiana na kuziendeleza.

Balozi huyo alipokelewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ambapo walifanya mazungumzo kwa ajili ya kuzitambulisha fursa zilizopo ndani ya mkoa huo.

Balozi Mtumbwide alisema Tanzania na Msumbiji zimekuwa na uhusiano wa muda mrefu na hivyo serikali za nchi hizo mbili zinatakiwa kushirikiana kuimarisha uhusiano huo ambao ulikuwapo hata kabla ya uhuru.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya aliona fursa za uwekezaji kwenye kilimo, biashara na viwanda vya kuchakata bidhaa mbalimbali.

“Uhusiano wa mataifa yetu ni wa muda mrefu sana, hapa nimekuja kwa lengo la kuimarisha uhusiano wetu pamoja na kuangalia fursa ambazo tunaweza tukashirikiana kwenye uwekezaji,” alisema Mtumbwide.

Alisema wapo Watanzania wanaoishi Msumbiji na wapo raia wa Msumbiji ambao wanaishi Tanzania kutokana na mataifa hayo jirani kuwa na uhusiano mzuri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mkoa huo uko tayari kushirikiana na Serikali ya Msumbiji hasa kwenye mambo ya kiuchumi pamoja na diplomasia.

Alisema serikali ya mkoa huo inawakaribisha wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza ili kuinua uchumi na kuongeza ajira kwa vijana.

# Wakazi Busokelo walia mazao kuharibikia shambani

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

ASILIMIA 40 ya mazao ya wakulima katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe mkoani Mbeya, huharibika yakiwa mashambani kutokana na kushindwa kusafirishwa kwa sababu ya ubovu wa miundombinu ya barabara hasa kipindi cha mvua.

Mazao ambayo huharibika chai, ndizi, maparachichi, viazi mviringo na mahindi ambayo ndiyo mazao yanayolimwa zaidi wilayani humo.

Hayo yalielezwa juzi na wakazi wa wilaya hiyo wakati wa hafla ya makabidhiano ya mradi wa ujenzi wa barabara ya kuanzia makao makuu ya halmashauri hiyo Lwangwa hadi Kyejo mahali ulipo mgodi wa gesi.

Barabara hiyo ina urefu wa kilomita sita na inaunganisha halmashauri hiyo na eneo ulipo mgodi wa kuchimba gesi asilia wa Kyejo ambapo barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mmoja wa wananchi hao, Asabwile Supole, alisema kipindi cha mvua barabara hiyo huwa haipitiki kabisa kutokana na aina ya udongo uliopo ambao huwa unateleza na kusombwa kirahisi na maji ya mvua.

Alisema wakulima huwa wanalazimika kusafirisha mazao yao kwa kujitwisha kichwani jambo ambalo ufanisi huwa mdogo na hivyo baadhi ya mazao huharibika yakiwa shambani.

“Hii barabara ni muhimu sana kwetu lakini imekuwa ikiharibika sana kipindi cha mvua, mazao haya yanapoharibika tafsiri yake ni kwamba uchumi wetu unaharibika,” alisema Supole.

Bupe Malamla aliishukuru serikali kwa kuamua kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami akidai kuwa mbali na kurahisisha usafirishaji wa mazao yao pia utapunguza gharama za usafirishaji wa mazao.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba barabara hiyo kujengwa lakini utekelezaji wake umechukua muda mrefu kutokana na kila mwaka kutotengewa bajeti.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Wilaya Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Wilson Charles, alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia sasa hivi mpaka kukamilika kwake.





# Wauguzi wadaiwa kusababisha kifo mama, mtoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya serikali kupunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi, lakini baadhi ya watendaji afya katika wodi za wazazi wanadaiwa kukwamisha juhudi hizo kutokana na uzembe wa kutotoa huduma kwa haraka.

Uzembe huo umesababisha kifo cha Kidawa Haji Khamis (35) ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Kidongochekundu na mtoto wake katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja Mjini Unguja wakati akijifungua.

Tukio hilo ambalo limetokea Machi 15, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi hospitalini hapo.

Akizungumzia na Nipashe, mume wa marehemu, Nassor Omar Khamis, aliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria wahudumu wa afya waliosababisha kifo hicho cha kumpoteza mke pamoja na mtoto kutokana na uzembe.

"Tunajua kuwa kifo kipo na kila mmoja atakufa lakini kifo hiki cha mke wangu na mtoto wangu kimetokana na uzembe wa wataalamu wa afya ambao waliokuwa na dhamana katika wodi ya wazazi ambapo tulimfikisha mke wangu kwa ajili ya kujifungua," alisema.

Salha Saleh Kassim ambaye ni wifi wa marehemu, alisema kabla ya kifo cha wifi yake walimfikisha hospitalini hapo majira ya saa tano asubuhi kwa ajili ya kujifungua.

Alisema walipofika hospitali hapo wahudumu walitelekeza licha ya kuomba msaada.

"Wakati tupo wodini Kidawa alianguka chini wakati akihangaika kutaka kujifungua bila ya kupata msaada kutoka kwa wataalamu wa afya, hawa wahudumu walituonesha dharau kubwa huu ni uzembe wa hali ya juu,"alisema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alifika katika Kijiji cha Dimani na kusema serikali itachukua hatua stahiki kwa waliohusika.

Waziri huyo aliitaka Wizara ya Afya, kufanya uchunguzi wa tukio hilo na kusema atakayebainika sheria itachukua mkondo wake.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwasimamisha kazi wafanyakazi waliohusika kusababisha kifo cha mzazi na mtoto huyo.

Pia alimtaka Katibu Mkuu Wizara ya Afya kuyaagiza mabaraza husika kufanya uchunguzi wa kina juu ya suala hilo na ripoti iwe imekamilika ndani ya siku saba.

Alisema amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha mama huyo ambaye alifika kujifungua katika hospitali hiyo.

Waziri huyo alisema sekta ya afya ina uwezo wa kupunguza vifo vya mama na mtoto na kuwahifadhi kinamama na watoto wasipate shida wakati wa kujifungua ikiwa wafanyakazi kila mmoja atafanya wajibu wake ipasavyo.

Aidha, uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja umewasimamisha watumishi waliohusika na tukio hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Muhiddin Abdi Mahmoud, alisema uongozi umeamua kuchukua hatua hiyo baada ya kutoridhishwa na kitendo hicho na kwamba hatua zingine za kiutumishi zitachukuliwa baada ya mabaraza kukaa na kujiridhisha.




Waziri wa Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe (kulia), na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita wakishiriki kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yadhamiria kuleta mageuzi sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema dhamira yake ni kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa mradi wa kuwajengea uwezo vijana wenye lengo la kuwawezesha kujiajiri kwenye sekta ya uchumi wa buluu.

Dk. Mwinyi alisema serikali inaendeleza jitihada ya kuhakikisha inatoa elimu bora katika kufikia dhamira hiyo kwa kuchukua hatua za kuboresha miundombinu ya shule, ikiwamo ujenzi wa shule mpya za ghorofa kwa Unguja na Pemba na mafunzo kwa walimu.

Alisema serikali itahakikisha inazipatia huduma muhimu shule hizo ikiwamo upatikanaji wa vifaa bora vya kufundishia na kujifunza, matumizi bora ya TEHAMA.

Dk. Mwinyi alitaja sehemu ya ujenzi wa mradi huo ni pamoja na chuo cha kisasa cha ubaharia na majengo ya utawala, ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike kwenye Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume yenye ukubwa wa ghorofa tatu na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 kwa wakati mmoja.

Lingine ni ujenzi wa madarasa ya kusomea na karakana zinazohusiana na masomo ya mafuta na gesi.

Alisema ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali na vifaa vyote vinavyohitajika kwa programu zitakazotolewa na vyuo hivyo ambavyo vinatarajiwa kujengwa kwenye wilaya za mkoani (Chambani), Wilaya ya Micheweni (Tumbe Mashariki), Wilaya ya Kati (Jendele) na Wilaya ya Kaskazini B (Panga Tupu).

Shughuli zingine ni kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi zinazoshiriki kwenye mradi huo kwa kuwapatia nafasi za kuongeza taaluma zao, ujenzi wa kituo cha kuwapa vijana mafunzo ya kuanzisha na kuendeleza biashara zao na vifaa vyake eneo la Kizimbani Unguja.

Dk. Mwinyi alisema hatua hiyo inatoa nafasi kwa vijana wa Zanzibar kupata fursa ya mafunzo ya amali na ufundi wa fani mbalimbali zikiwamo zinazohusiana na uchumi wa buluu.

Pia aliwataka vijana kuitumia vyema fursa ya mradi huo kujipatia ujuzi ili wanufaike na soko la ajira kwenye sekta ya uchumi wa buluu kwa kujiajiri na kupata sifa za kuajiriwa.

Dk. Mwinyi alisema mradi huo utaongeza upatikanaji wa wafanyakazi wenye taaluma kwenye shughuli za utalii ambayo ni sekta kiongozi katika uchumi wa Zanzibar pamoja na kuiwezesha Zanzibar kuzitumia vyema rasilimali zake za asili ikiwamo bahari, mafuta na gesi asilia katika kukuza pato la taifa na upatikanaji wa ajira kupitia sekta ya uchumi wa buluu.

Mradi wa kuwajengea uwezo vijana kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri kwenye sekta ya uchumi wa buluu unafadhiliwa kwa asilimia 90 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na asilimia 10 unafadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, unatarajiwa kutumia Dola milioni 54 (Sh. bilioni 126.3).

# Waziri Mkuya: Sekta ya fedha, benki zimeimarika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya amesema, sekta ya fedha na benki zimeendelea kuimarika na kuchangia kuwapo kwa utulivu wa bei na kusaidia ukuaji endelevu wa uchumi.

Alisema ripoti ya usimamizi wa sekta ya fedha ya mwaka 2021 ilionyesha kwamba sekta hiyo imeendelea kuwa imara na ukwasi wa kutosha licha ya matatizo mbalimbali yaliyojitokeza duniani.

Aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakih aliyetaka kujua ni ipi tathmini ya kitaalamu ya karibuni ya mfumo wa fedha na benki ulioangalia ukuaji bora wa uchumi wa Zanzibar.

Waziri Mkuya alisema katika kipindi cha miaka mitano (2018 - 2022), sekta ya fedha na benki ilichangia wastani wa asilimia 3.5 ya pato la taifa la Zanzibar.

"Sekta hii ilichangia kiasi kama hicho kwa upande wa Tanzania Bara. Mtandao wa matawi ya benki, mawakala na miamala kwa njia ya simu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, ambapo hadi mwishoni mwa mwaka 2022, kwa upande wa Zanzibar kulikuwa na benki 14, zenye mtandao wa matawi 36, na mawakala 1,555," alisema.

Aidha, alisema kuanzia Julai hadi Desemba 2022, amana zilizokusanywa na benki zilizopo Zanzibar ilifikia Sh.bilioni 1.5 kutoka Sh. bilioni 1.2 zilizokuwapo kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia.

Alisema pia mikopo iliyotolewa ilifikia Sh. bilioni 1.8 ambayo ni ongezeko la asilimia 44.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia.

Waziri huyo alisema jukumu la msingi la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kama ilivyoainishwa katika ibara ya 5 na 7 ya Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 2006 ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga uwepo wa utulivu wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa.

Alisema: "Benki Kuu ya Tanzania huandaa sera ya fedha kwa kila mwaka wa fedha wa serikali kulingana na malengo mapana ya kiuchumi yanayowekwa na serikali zote mbili, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia (SMT)na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) pamoja na mipango na sera za serikali zote mbili".

Waziri Mkuya alisema malengo mapana ya kiuchumi hujumuisha ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, mapato na matumizi ya serikali na akiba ya fedha za kigeni.

# Wenyeviti vitongoji wasotea posho miaka minne

**Na Anthony Gervas, MAGU**

WENYEVITI wa vitongoji katika kijiji cha Kisesa kata ya Bujora, Magu mkoani Mwanza, wanailalamikia halmashauri ya wilaya hiyo kushindwa kuwalipa posho kwa miaka minne sasa tangu mwaka 2019 walipochaguliwa.

Malalamiko hayo waliyatoa jana baada ya halmashauri hiyo kwenda katika vitongoji vyao na kuwalipa Sh. 18,000 kila mmoja badala ya Sh. 144,000 wanazodai kila kiongozi kwa kipindi cha miaka minne, jambo ambalo wamesema limegeuka kuwa kero kwao.

Wenyeviti hao ni Michail Bogohe wa kitongoji cha Iseni- Mlimani, Ng'wenesho Malago wa kitongoji cha Ng'wang'halanga 'A' Philip Chambwite wa kitongoji cha Ng'wang'halanga. Walisema hawatendewi haki kama wanavyotendewa madiwani, wabunge na viongozi wengine wa kuchaguliwa.

"Halmashauri ya Wilaya ya Magu tunaidai posho zetu kwani haijatulipa miaka minne sasa toka tuchaguliwe mwaka 2019. Kila mmoja tunadai shilingi 144,000 lakini mwezi huu tumeletewa Sh. 18,000 kila mtu wakati tunafanya kazi kubwa usiku na mchana bila kupumzika," walisema.

Walisema inashangaza serikali kushindwa kuwalipa kiasi hicho cha fedha wakati ni kidogo na hutakiwa kulipwa kila mwezi Sh. 3,000 na kwamba kwa hesabu kila siku wanafanya kazi kwa Sh, 100 huku wakiomba kuongezewa kiwango cha posho hadi Sh. 5,000 kwa mwezi.

Kazi wanazozifanya saa 24 bila kulala, walisema ni pamoja na ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao kwenye vitongoji, kutatua migogoro ya ndoa, mipaka ya ardhi kwa jamii, kuhamasisha shughuli za maendeleo ya wananchi ikiwamo kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Aidha waliiomba serikali kuwatazama kwa jicho la huruma pindi wanapomaliza muda wao madarakani wa miaka mitano kwa kuwalipa mafao ya kiinua ngongo kama wanavyolipwa madiwani,wabunge na viongozi wengine.

Akitoa ufafanuzi ofisini kwake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Fidelica Myovella, alisema bado hajapata malalamiko ya wenyeviti hao.

"Sisi halmashauri huwa tunalipa posho hizo wakati mwingine kila baada ya miezi mitatu au vyovyote vile. Hakuna kumbukumbu yoyote ofisini kwangu ya malalamiko ya kutolipwa wenyeviti wa vitongoji wala mtaa inayohusu madai ya miaka minne. Labda madai ya nyuma kabla sijaja hapa, walete malalamiko yao ofisni," alisema Myovella.

Alisema wenyeviti hao kuyapeleka katika vyombo vya habari ni sahihi lakini wampelekee na yeye ofisini kwake ili kuzungumza na kupata ufumbuzi.

# CRDB yatia mkono usalama kwa watalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeipongeza Benki ya CRDB kwa kutoa msaada wa pikipiki 15 kwa Jeshi la Polisi mkoani Arusha, ili kuimarisha doria zitakazoongeza usalama kwa watalii wanaokuja nchini.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Waziri wa Utalii na Maliasili, Mohamed Mchengerwa, alipopokea pikipiki hizo zenye thamani ya Sh. milioni 40 kwenye hafla fupi iliyofanyika katika Kituo cha Polisi cha Utalii na Diplomasia jijini hapa.

Waziri alisema sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika uchumi na maendeleo ya wananchi nchini na kwamba inayoongoza kwa kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni, ikiwa ya pili kwa kuchangia kwenye Pato la Taifa (GDP), na ya tatu kwa kutoa ajira.

"Ripoti za Benki Kuu Tanzania (BoT) zinaonyesha sekta ya utalii inaendelea kuimarika baada ya kuathiriwa na janga la UVIKO-19.

"Mapato yatokanayo na utalii kwa Machi yalifikia Dola za Marekani bilioni 2.787 ikilinganishwa na dola milioni 885 kipindi kama hicho mwaka 2021. Katika mwezi huo, watalii 1,574,630 waliingia nchini," alisema.

Aidha, Mchengerwa alipongeza jitihada zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuitangaza Tanzania kupitia filamu ya The Royal Tour.

"Kipeeke kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa msaada huu wa pikipiki 15 ambao Benki yetu ya CRDB imeutoa kwa kituo chetu hiki.

"Pikipiki hizi zitawawezesha askari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Askari watakabiliana haraka na dharura jambo litakalosaidia kuimarisha usalama kwa watalii na kuifanya nchi yetu kuwa kivutio kikubwa hivyo wageni wengi kuja kuitembelea," alisema.

Alisema mwaka 2020, sekta ya utalii ilichangia asilimia 10.6 kwenye pato la taifa ila kiasi hiki kilishuka hadi asilimia 5.7 mwaka 2021 kutokana na athari za UVIKO-19, na kuilazimu serikali kuchuku ahatua za makusudi kuifufua kwa kufuata taratibu za Shirika la Afya Duniani (WHO) na kufanya matangazo kimataifa kwa Rais Sami.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, ili kuhakikisha usalama wa watalii wanaokuja nchini, serikali ilianzisha kitengo maalum cha utalii na diplomasia kwa ajili ya kuwahudumia watalii na wanadiplomasia wanaofika nchini kutalii ama kuwekeza kwa haraka.

"Kwa kuwa jiji la Arusha ndilo kitovu cha utalii nchini, kituo hicho kimejengwa huko na askari wake walipewa mafunzo ya ziada ndani na nje ya nchi juu ya namna bora ya kuhudumia watalii. Vituo vingine vidogo vimefunguliwa katika wilaya za Arumeru, Karatu, Monduli na Longido," alisema.

Akikabidhi pikipiki hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kila mmoja anafahamu umuhimu wa amani, utulivu na usalama katika maendeleo ya nchi kiuchumi, kijamii na kisiasa hivyo ni jukumu la jamii nzima kushiriki kuuimarisha.

"Pamoja na kuwapo hali ya amani na utulivu nchini, bado baadhi ya matukio ya uhalifu hujitokeza kama vile vile uporaji wanaofanyiwa raia hata watalii wanaokuja kutembelea vivutio vilivyopo nchini. Ili Jeshi la Polisi litekeleze majukumu yake kwa ufanisi linahitaji vitendea kazi vya kutosha," alisema Nsekela.

Mkurugenzi huyo alisema benki hiyo inafurahi kwa kuwa pikipiki hizo zitawasaidia askari kufuatilia wahalifu wanaowapora watalii au kusafirisha mihadarati hivyo kuharibu sifa njema za jiji hili la kitalii.

"Tunaamini matumizi sahihi ya pikipiki hizi yatasaidia kudhibiti uhalifu jijini hapa na tunaahidi tutaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi nchini kupunguza baadhi ya changamoto zinazokwamisha ufanisi wake ili nchi yetu iendelee kuwa salama kwa biashara na uwekezaji," alisema Nsekela.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Edith Swebe, alisema jitihada zinazoendelea kuutanga utalii wa Tanzania umelifanya Jiji la Arusha kupokea wageni wengi wanaoongeza haja ya askari polisi kuwapo katika kila eneo.

"Tunachokifanya sasa hivi ni kusimamia mradi wa utalii salama ambao unahitaji askari kuwapo kila walipo wageni. Pikipiki hizi tunazozipokea zitasaidia kuwafikisha askari kwenye maeneo ambako magari hayawezi kufika kwa urahisi zikiwamo barabara nyembamba. Jeshi la Polisi linaamini mazingira salama ni kivutio cha utalii," alisema Edith ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa kamanda wa Mkoa wa Simiyu.




Mkurugenzi wa Taasisi inayotoa elimu ya uongozi ya Toastmasters International Afrika Mashariki, Emilia Siwingwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano wa mwaka wa taasisi hiyo wa siku mbili unaoanza leo. Kulia ni Rais wa Taasisi hiyo, Matt Kinsey. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yafanya utafiti haja mabadiliko sheria kujamiiana

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema inaendelea kutekeleza maelekezo ya Bunge kufanya utafiti zaidi ili kuona kama kuna hitaji la kufanya marekebisho ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kuhusu makosa ya kujamiiana.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itawasilisha Muswada wa Sheria ya Adhabu kali kwa wanaobaka na kulawiti watoto na wanawake.

Akijibu swali hilo, Gekul alisema kwa mujibu wa vifungu 130, 131, 131A na 154 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, ni makosa ya jinai kwa mtu kubaka na kulawiti na makosa yote haya adhabu yake ya juu ni kifungo cha maisha jela na adhabu ya chini ni kifungo cha miaka 30 jela.

Pia alisema kwa makosa yote hayo yakitendeka dhidi ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 10, adhabu yake ni kifungo cha maisha jela.

"Pamoja na adhabu hizo, mahakama ina mamlaka ya kutoa amri ya ziada ya kumlipa fidia mwathirika chini ya kifungu cha 131(1) cha Kanuni za Adhabu,"alisema.

HABARI KIMATAIFA

# Wanasayansi: Joto kuongezeka kwa asilimia 98 duniani

**GENEVA, Uswisi**

WANASAYANSI wameonya kuwapo kwa viashiria vya joto kupita kiasi kutoka asilimia 60 hadi 98 duniani na huenda kupita kikomo muhimu cha halijoto kwa mara ya kwanza katika miaka michache ijayo.

Watafiti wanasema sasa kuna uwezekano wa asilimia 66 ya kuvuka kiwango cha ongezeko la joto la 1.5C kilichopo sasa na kuongezeka mwaka 2027.

Wanatabiri takwimu hizo zitaongezeka zaidi na kwa uhakika wa asilimia 98 kiwango cha juu zaidi kitafikiwa kabla ya mwaka 2027.

Uwezekano huo, unaongezeka kutokana na hewa chafu kutokana na shughuli za binadamu na hali ya hewa ya El Nino baadaye mwaka huu.

Kufikia kiwango hicho kunaweza kumaanisha kuwa dunia ina joto la 1.5C kuliko ilivyokuwa katika nusu ya pili ya Karne ya 19, kabla ya uzalishaji fueli za visikuku kutokana na ukuaji wa viwanda kuanza kuongezeka.

Kiwango cha joto cha 1.5C imekuwa ishara ya mazungumzo ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

Nchi zilikubali kuendeleza juhudi za kupunguza viwango vya joto duniani hadi 1.5C chini ya makubaliano ya mwaka 2015 huko Paris, Ufaransa, huku athari zikitajwa dhoruba kali zaidi na moto wa nyikani.

Wanasayansi wanasema bado kuna wakati wa kuzuia ongezeko la joto duniani kwa kupunguza uzalishaji wa hewa chafuzi kwa mazingira.

Tangu 2020 Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), limekuwa likitoa makadirio ya dunia kupita kiwango cha nyuzijoto cha 1.5C katika mwaka wowote ule.

Hapo nyuma walitabiri kulikuwa na chini ya asilimia 20 ya uwezekano wa kupita kiwango hichi cha 1.5C katika miaka mitano ijayo.

Kufikia mwaka jana, hali ilikuwa imeongezeka hadi asilimia 50, na sasa imepita hadi asilimia 66, ambayo wanasayansi wanasema inamaanisha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutokea.

Mwaka 2016, joto kurekodiwa kimataifa ilikuwa nyuzi 1.28C takwimu hizo zikiwa za juu ya kabla ya viwanda.

"Kwa kweli sasa tuko ndani ya uwezekano wa kupita kiwango cha joto 1.5C kwa muda mfupi kwa mwaka, na hiyo ni mara ya kwanza katika historia ya wanadamu kuwa karibu kiasi hicho," Prof Adam Scaife, Mkuu wa Utabiri wa Masafa Marefu, WMO.

*BBC*



Aline Niyokwizera, kutoka kusini mwa nchi ya Burundi akizungumza na vyombo vya habari, kwenye uwanja wa ndege wa Bujumbura muda mfupi kabla ya mabinti hao kuondoka. **PICHA: BBC**

# Watoto 4 wakutwa hai siku 16 baada ya ajali ya ndege

**ARARACUARA, COLOMBIA**

MAOFISA nchini Colombia, wanasema watoto wanne waliotoweka tangu ndege kuanguka msituni, wamepatikana wakiwa hai zaidi ya wiki mbili baadaye.

Mama yao na watu wazima wengine, walifariki katika ajali hiyo.

Shirika la Serikali la Ustawi wa Watoto (ICBF), lilisema limepata taarifa kutoka eneo hilo kwamba, watoto hao wamepatikana wakiwa na afya njema.

Rubani alisema pia alikuwa ameambiwa watoto hao wamepatikana na watu wa kiasili ndani ya msitu huo mkubwa.

Wanajeshi wanaoshiriki katika msako huo, hata hivyo, bado hawajawaona watoto hao.

Ndege hiyo ndogo aina ya Cessna 206 waliyokuwa wakisafiria, ilikuwa ikisafiri kutoka Araracuara, ndani kabisa ya msitu wa Amazon, kusini mwa Colombia, kuelekea San José del Guaviare, ilipotoweka asubuhi ya Mei Mosi, mwaka huu.

Rubani alikuwa ameripoti mapema matatizo ya injini.

Baada ya msako mkubwa uliohusisha zaidi ya wanajeshi 100, hatimaye ndege hiyo ilipatikana Jumatatu, wiki mbili baada ya kutoweka.

Miili ya rubani, rubani msaidizi na Magdalena Mucutuy mwenye umri wa miaka 33, mama wa watoto hao wanne, ilipatikana katika eneo la ajali katika jimbo la Caqueta.

Lakini watoto hao, ambao wana umri wa miaka 13, tisa na minne, pamoja na mtoto mchanga wa miezi 11, hawakupatikana.

*BBC*

## Kenyatta kuongoza ujumbe EAC, Goma

**NAIROBI, Kenya**

UJUMBE kutoka Ofisi ya Mratibu wa mazungumzo ya Amani Mashariki mwa DRC kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta, unatarajiwa kuzuru Goma, kutathmini maendeleo ya hali ya usalama.

Hatua hiyo inajiri siku chache baada ya Rais Felix Thisekedi, kunukuliwa akisema hajafurahishwa na utendaji kazi wa kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kuhusu kinavyokabiliana na waasi wa M 23.

Haijawa wazi iwapo Kenyatta naye atakuwa miongoni mwa wajumbe hao, ambao kazi yao itakuwa ni kuandaa ripoti itakayowasilishwa kwa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wanaotarajiwa kukutana baadae mwezi huu, kujadili hali ya usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wajumbe hao watatathmini mafanikio na changamoto za kikosi cha EAC, ambacho kilitumwa mwaka uliopita, kusaidia kuleta amani na kuwaondoa waasi wa M 23 katika maeneo ambayo walikuwa wanadhibiti.

Ziara hiyo inakuja katika kipindi ambacho kikosi hicho kimepata Kamanda mpya, Meja Jenerali Alphaxard Kiugu, kutoka Kenya, baada ya kuondoka kwa mtangulizi wake, Meja Jenerali Jeff Nyagah.

*RFI*

## Wasafirishwa Saudia kufanya kazi za ndani

**BUJUMBURA, Burundi**

MABINTI 11 wa Burundi wamesafiri kutoka uwanja wa ndege wa Bujumbura, kuelekea Saudi Arabia kufanya kazi za nyumbani katika mpango wa serikali za nchi hizo, zinazounga mkono mpango wa kuzuia uhamaji haramu wa wafanyakazi.

Mamia ya wanawake wa Burundi, wengi wao wakiwa wasichana wadogo, wamesafirishwa na makampuni ya biashara kwenda kufanya kazi za nyumbani katika nchi za Kiarabu na baadhi yao walisema, walivumilia ukatili wa nyumbani uliokithiri.

"Nina furaha sana...baada ya takribani miaka minne ya kukosa kazi," Aline Niyokwizera (22), kutoka kusini mwa Burundi alisema kabla ya kuondoka uwanja wa ndege wa Bujumbura.

Sitini kati yao, wote wakiwa wamevalia mavazi ya wanawake wa Kiislamu, walikuwa kwenye uwanja wa ndege tayari kuondoka lakini 11 pekee, ndio waliokwenda.

Waliosalia watasafiri siku ya Ijumaa, baada ya kukosa viti kwenye ndege ya Jumatano jioni.

*BBC*

# SHIKANGWA MFUNGAJI BORA LIGI YA WANAWAKE 2022/23

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI JKT Queens ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara kwa msimu wa 2022/2023, straika wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa ameibuka Mfungaji Bora baada ya kupachika mabao 17.

Straika huyo raia wa Kenya alihitimisha hesabu zake kwa kufunga bao pekee kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa, Iringa timu yake ilipocheza dhidi ya wenyeji Mkwawa Queens.

Shikangwa ambaye alisajiliwa katika dirisha dogo la usajili Desemba, mwaka jana amekuwa msaada mkubwa kwenye timu yake iliyomaliza nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi 45, moja pungufu dhidi ya mabingwa, JKT Queens.

Mchezaji huyo anafuatiwa na Winfrida Charles wa Alliance Girls ya Mwanza ambaye amefunga mabao 13, Donisia Minja wa JKT Queens mwenye mabao 12 anashika nafasi ya tatu akifuatiwa na Stumai Abdallah wa JKT Queens pia mwenye magoli 10.

JKT Queens ilimaliza ligi hiyo yenye timu 10 kwa kishindo, ikiisasambua Mkwawa Queens mabao 7-2 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Samora, mjini Iringa.

JKT Queens inachukua ubingwa huo na kumaliza utawala wa Simba Queens ambayo iliuhodhi kwa misimu mitatu mfululizo.

Ilikuwa inahitaji ushindi tu kwenye mechi hiyo dhidi ya timu dhaifu, Mkwawa Queens iliyoshuka daraja.

Kwa ubingwa huo, sasa itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) itakayochezwa kuanzia Juni 3 hadi 17, mwaka huu huko Kenya ili kusaka mwakilishi wa ukanda huu atakayekwenda katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba Queens imeukosa ubingwa kwa kushindwa kuifunga JKT Queens msimu huu, mechi ya kwanza ambayo ndiyo imewaathiri ilifungwa mabao 2-1, kwenye Uwanja wa Mo Arena, Desemba 6, mwaka jana ambayo ilikuwa ni ya ufunguzi wa ligi na Machi 10, mwaka huu waliporudiana, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 , mechi ikichezwa Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (kulia), akizungumza na vijana kutoka katika makundi mbalimbali ya jogging, Dar es Salaam kwa lengo la kuwakumbusha kujiheshimu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mitihani yasogeza Ligi ya Kabaddi

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Kabaddi Tanzania (TKSA) kimetangaza kusogeza mbele Ligi ya Taifa ya mchezo huo ambayo sasa itachezwa kuanzia Mei 30 hadi Juni Mosi, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa TKSA, Abdallah Nyoni, alisema awali ligi hiyo ilipangwa kufanyika kuanzia leo lakini wamelazimika kufanya mabadiliko kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje ya chama hicho.

Nyoni alitaja sababu mojawapo ni wadhamini wakuu wa ligi hiyo kutumia ukumbi kwa ajili ya mitihani ambayo inaendelea.

"Maandalizi yanaendelea kufanyika kuhakikisha ligi inachezwa kwa weledi kwa sababu itatumika kuchagua nyota watakaounda Timu za Taifa za wanawake na wanaume zitakazoshiriki michuano ya kimataifa.

Hapa chuo ndio wadhamini wetu wa eneo la kufanyia ligi yetu, sasa hivi kuna mitihani inaendelea, hivyo hatuwezi kuendesha mashindano, tuziomba timu shiriki kutumia muda huu kujiimarisha zaidi," alisema Nyoni.

Aliongeza timu zilizothibitisha kushiriki ligi hiyo mpaka sasa ni sita za wanawake na wanaume na zinatoka Tanzania Bara na Zanzibar ambao nao wanashiriki.

Alizitaja timu hizo ni Buffalo Kabaddi SC, Kaole Kabaddi, Mt.Kilimanjaro, Star Kabaddi, St. Joseph University Kabaddi na KMKM SC kutoka Visiwani Zanzibar.

# Jogging waaswa kujiepusha ngono

**Na Sabato Kasika**

WANAMICHEZO wametakiwa kuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vya ukatili ikiwamo rushwa ya ngono ili kuwa na wanamichezo watakaosaidia kuliletea taifa sifa njema.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, wakati akizungumza na makundi ya Jogging ya Talent, Smart na Wanaka ya Tabata, Dar es Salaam.

Mawinza alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeenea sehemu zote ikiwamo hata katika makundi ya jogging na vijana wa makundi hayo hawana budi kujiweka mstari wa mbele kukemea.

"WAJIKI tunaendesha kampeni 'Safiri Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', kwa lengo la kukomesha ukatili wa kijinsia na leo (jana), tumekuja kwenu kuwaomba mtuunge mkono," alisema Mawinza.

Aliongeza ukatili huo umekuwa ukifanyika kwa watoto na vijana wakike na kiume wakiwamo waliomo kwenye makundi ya jogging, na ni muhimu makundi hayo yakapambana na vitendo hivyo.

"Mnapokutana katika mazoezi au sehemu nyingine, ni muhimu mkawa mnaelimishana, ili kila mmoja wenu atambue madhara ya rushwa ya ngono na kuiepuka asifanyiwe wala kumfanyia mwenzake," kiongozi huyo alisema.

Alisema WAJIKI imekuwa ikifanya kampeni shuleni, vijiwe vya madereva wa bodaboda, daladala na hata ndani ya jamii, na sasa wameamua kuwafuata wanamichezo.

"Women Fund Tanzania (WFT), wametufadhili katika kazi hii, lengo ni kutaka jamii yote inakuwa na uelewa kuhusu madhara ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia kwa ujumla wake,"alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza shirika lake linaamini safari salama bila rushwa ya ngono inawezekana, iwapo jamii yote itahamasika na kujitokeza kupinga vitendo hivyo bila kificho.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMNG'OA RICE

ARSENAL inatayarisha ofa ya pauni milioni 92 kwa kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, ambayo itakuwa uhamisho wa rekodi ya klabu. ***(Telegraph)***

### TUCHEL: NAMTAKA RICE

KLABU ya Bayern Munich pia wanavutiwa na Declan Rice huku bosi wake Thomas Tuchel akitafuta kuimarisha safu yake ya kiungo. ***(Mirror)***

### CANCELO ATAKIWA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta pia ana nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa yuko Bayern Munich kwa mkopo, lakini Arsenal wanahofia City watasita kufanya biashara nao msimu huu wa joto. ***(Sport)***

### PSG YAMTAKA SILVA

KLABU ya Paris St-Germain wanataka kumsajili Bernardo Silva wa Manchester City mwenye umri wa miaka 28, baada ya kushindwa kumpata kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno msimu uliopita. ***(Telegraph)***

### KLOPP AMBEBA MILNER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alitaka kumbakisha kiungo wa kati wa England, James Milner, mwenye umri wa miaka 37, na kumpa mkongwe huyo nafasi ya ukocha katika klabu hiyo. ***(Mirror)***

### UNITED, KIM MAMBO SAFI

KLABU ya Manchester United imekubali makubaliano ya kibinafsi na beki wa Napoli mwenye umri wa miaka 26, Kim Min-jae. ***(Il Mattino, via Metro)***

### ODEGAARD KUJIFUNGA TENA

KIUNGO wa kati wa Arsenal na Norway, Martin Odegaard anatazamiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ukikamilika 2025. ***(90min)***.

### ALONSO KUBAKIA LEVERKUSEN

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso amethibitisha bado ataendelea kuinoa klabu hiyo ya Ujerumani msimu ujao baada ya kiungo huyo wa zamani wa Liverpool kuhusishwa na nafasi ya ukocha iliyo wazi ya Tottenham Hotspur. ***(Sky Sports)***

### LOKONGA KUMFUATA KOMPANY

MCHEZAJI wa Arsenal, Albert Sambi Lokonga, mwenye umri wa miaka 23 anaweza kutaka kuhamia Burnley ili kuungana na Kocha, Vincent Kompany, ambaye alimfundisha Mbelgiji huyo katika alipokuwa anaiongoza Anderlecht. ***(Express)***

### ZAHA KUBAKIA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha, anafikiria kusalia Crystal Palace, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ukimalizika msimu huu wa joto. ***(Sports)***

### ZUBIMENDI ANUKIA BARCA

KLABU ya Barcelona itafanya jaribio jipya la kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi, mwenye umri wa miaka 24 msimu huu baada ya Arsenal kuripotiwa kushindwa na ofa ya pauni milioni 53 mwezi Januari. ***(Express)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATAMBA SASA NI ZAMU YAO

Ni kutokana na kuipa kichapo cha bila huruma Madrid katika...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City inasherehekea kurejea fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwafunga mabingwa watetezi, Real Madrid kwa kufanya vyema katika historia ya klabu hiyo.

Kikosi cha Pep Guardiola kinachofukuzia mataji matatu kiliwafunga mabao 4-0 mabingwa hao mara 14 wa Ulaya katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad juzi, na kukata tiketi ya kutinga fainali itakayochezwa jijini Istanbul, Uturuki kwa ushindi wa jumla ya magoli 5-1.

Ushindi ulikuwa wa kuridhisha huku Madrid ikimshukuru golikipa, Thibaut Courtois, kwa kuzuia hatari zaidi kwao.

Bernardo Silva aliiweka City kwenye njia ya kutinga fainali dhidi ya Inter Milan kwa mabao mawili ya kipindi cha kwanza kabla ya Eder Militao kujifunga na Julian Alvarez kuongeza la nne mwishoni mwa mchezo.

City sasa watatumaini kunyanyua kombe hilo na kufanya marekebisho kwa kupoteza kwao katika fainali ya 2021 kama sehemu ya kile ambacho kinaweza kuwa mataji matatu.

Taji la kwanza kati ya hayo linaweza kuja Jumapili ikiwa wataifunga Chelsea na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England na fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United itakayofanyika Juni 3, mwaka huu.

City Guardiola alisema: "Kwenye Ligi Kuu tumekaribia, tunajua tunahitaji mchezo mmoja zaidi. "Tunacheza dhidi ya majirani zetu na dhidi ya timu ya Italia katika fainali. Msimu ni mzuri sana. Tuko karibu na bila shaka tutajaribu."

Mechi ya nusu fainali ya kwanza ya wiki iliyopita dhidi ya Madrid iliyochezwa kwenye Uwanja wa Bernabeu ilikuwa na ushindani mkali, City walitawala umiliki wa mpira kwa muda mrefu lakini Real walikuwa makini zaidi katika mashambulizi ya kaunta.

Wakati huu City ilikataa kuwaruhusu wapinzani wao kukaa nyuma na kujisikia raha na kupata presha.

Ushindi huo mkubwa ulifanya kulipiza kisasi kwa City baada ya kupoteza dhidi ya Madrid katika hatua kama hiyo msimu uliopita.

Guardiola alisema: "Ilikuwa ngumu sana kupoteza jinsi tulivyopoteza. Wakati huo tulilazimika kumeza sumu lakini mpira wa miguu na michezo huwa inakupa nafasi nyingine.

"Wakati droo ilipokuwa Madrid, nilisema, 'ndio naitaka'.

"Kila kitu kilikuwepo, nguvu tuliyokuwa nayo kutoka kwa mwaka wa kukosolewa kama wachezaji kwa kutokuwa na tabia tulipopoteza."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,114,9

MECHI KALI
AL AHLY CAIRO
VERSUS
ESPERANCE TUNIS
1 | 1.86
X | 2.95
2 | 4.32

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# RASHFORD AREJEA MAZOEZINI UNITED

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford ameongeza matumaini ya Manchester United kumaliza katika nafasi ya nne bora kwenye Ligi Kuu England kwa kurejea mazoezini.

Mshambuliaji huyo wa England, Rashford, ambaye amefunga mabao 29 msimu huu, alikosa kwenye ushindi wa mabao 2-0 katika mechi iliyopita dhidi ya Wolves kutokana na jeraha la mguu.

"Kuna habari njema kuhusu Marcus Rashford na Scott McTominay, ambao wote wamerejea mazoezini," taarifa ya United ilisomeka baada ya kikosi cha kwanza cha Erik ten Hag kufanya mazoezi Carrington hapo juzi.

"Mfungaji wetu anayeongoza alishiriki kwenye mazoezi baada ya kukosa ushindi dhidi ya Wolves kutokana na jeraha."

Kiungo wa kati wa Scotland McTominay pia anakaribia kurejea, akiwa hajacheza tangu tangu Aprili 8, mwaka huu alipofunga bao katika ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Everton.

Beki wa Ufaransa Raphael Varane, ambaye Ten Hag alisema alibadilishwa baada ya kuchelewa dhidi ya Wolves kama tahadhari, pia alifanya mazoezi Jumatano.

Baada ya safari yao katika pwani ya kusini, United inahitimisha kampeni yao ya ligi kwa mechi za nyumbani dhidi ya Chelsea na Fulham.

# Bonucci ajiandaa kustaafu

**TURIN, Italia**

BEKI wa kimataifa wa Italia na Juventus, Leonardo Bonucci, amesema anatarajia kustaafu mwishoni mwa msimu ujao ikiwa mkataba wake ndani ya klabu hiyo utakapofikia mwisho.

Bonucci ambaye amekua kwenye klabu ya Juventus kwa muda mrefu akiitumikia timu hiyo na kushinda mataji mengi ametangaza kustaafu baada ya msimu ujao kumalizika atatundika daluga akiwa na umri wa miaka 37.


Beki huyo alisema hayo alipohojiwa na Mtandao wa You Tube wa klabu hiyo na kuongeza anakwenda kustaafu mwakani itakuwa ndio mwisho wa zama za uzuiaji kwa staili ya kiitaliano kama ambavyo walikua wakifanya wao na waliopita huko nyuma.

Bonucci ambaye ameitumikia Juventus michezo 500 mpaka sasa ameibua maswali kutokana na kauli yake hiyo ya kusema akistaafu yeye ndio utakua mwisho wa uzuiaji wa aina ya kiitaliano.

Hii imeonyesha beki huyo haoni beki mwingine wa Kiitaliano ambaye atafuata nyendo zao.

Bonucci atakumbukwa kwa mafanikio makubwa aliyoyapata ndani ya Juventus kama kushinda mataji kadhaa ya Serie A, Copa Italia, vilevile kucheza fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini pia beki huyo amefanikiwa kwenye ngazi ya timu ya taifa kwa kutwaa taji la Euro mwaka 2021 akiwa na Italia.



65,687/-

# MAKATA AFUNGUKA SABABU ‘ILIYOWAUA’ RUVU SHOOTING

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushuka daraja, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata (pichani), amesema kuna ‘mlolongo’ wa sababu mbalimbali zilizopelekea timu hiyo kushindwa kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inakaribia ukingoni, imeelezwa.

Mei 12, mwaka huu, Ruvu Shooting ilishuka daraja rasmi ilipokubali kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Simba, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kuifanya kusalia na pointi zake 20.

Kipigo hicho kiliisafirisha timu hiyo kutoka Ligi Kuu na kwenda Championship kwa sababu hata ikishinda mechi mbili zilizobaki itafikisha pointi 26 tu ambazo itakuwa imeipita timu moja tu ya Polisi Tanzania.

Makata alisema usajili wa wachezaji wasiokuwa na viwango vinavyoitakiwa kwa sasa ni sababu kuu iliyowafanya washindwe kuendana na ushindani uliopo.

“Vitu vingi vimesababisha timu ishuke daraja, ikiwamo usajili wa mwanzo wa msimu. Tulikosea kwenye kusajili, wakasajiliwa wachezaji ambao uwezo wao sio ule mkubwa wa kucheza Ligi Kuu. Siku hizi ligi imekuwa nguvu sana Tanzania, unatakiwa uwe na wachezaji wenye uwezo mkubwa, hata wachache ili kukabiliana na timu nyingine.

Timu nyingi kwa sasa zinasajili wachezaji wa hali ya juu. Uliona kwenye mechi dhidi ya Simba, mipango yote ilikuwa sahihi, lakini tulichozidiwa ni kiwango cha mchezaji mmoja mmoja,” alisema Makata.

Aliongeza hata kipindi cha dirisha dogo hakukuwa na fungu la usajili, badala yake walisajili mchezaji mmoja (Valentino Mashaka), tu hivyo ilikuwa ngumu kukabiliana na baadhi ya timu ambazo zimesajili na kuwekeza kwenye wachezaji bora.




## Rais Samia aipa ndege...

INATOKA UK. 24

“Ni faraja kubwa sana, msimu ulikuwa mrefu na tumefanya kazi sana, tumestahili kufika hapa, ila sasa tunapaswa kumalizia kule tunakopaswa kufika. Nawaambia wanachama na mashabiki Yanga hapa siyo mwisho, tumejipanga kumalizia,” alisema Kaze.

Mshambuliaji nyota wa timu hiyo ambaye juzi alifunga bao la kwanza na ‘assist’ ya goli la pili, Fiston Mayele, alisema anaamini wanaweza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kutokana na kikosi kizuri walichonacho.

Yanga imetinga fainali baada ya ushindi wa jumla wa mabao 4-1 wakati wapinzani wao, USM Alger waliwachapa ASEC Mimosas magoli 2-0, baada ya suluhu ya ugenini.

## Simba yatangaza dk. 180 za furaha

INATOKA UK. 24

wake watapambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo hiyo kwa lengo la kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo ambao waliwasapoti wakati wote.

Alisema pia mipango kuelekea msimu mpya imeshaanza na wanawaahidi mashabiki watawafuta machozi kutokana na kushindwa kufikia malengo msimu huu.

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/05/23 | 17:00 | Fulham FC vs Crystal Palace | 2.33 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 20/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Everton FC | 2.55 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 20/05/23 | 17:30 | FC Arouca vs GD Chaves | 2.44 | 3.25 | 2.70 |
| 04. 20/05/23 | 18:00 | FC Nantes vs Montpellier HSC | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 05. 20/05/23 | 19:15 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.27 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 20/05/23 | 22:00 | Lille OSC vs Olympique Marseille | 2.25 | 3.45 | 2.80 |
| 07. 21/05/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Fluminense FC RJ | 2.65 | 3.30 | 2.44 |
| 08. 21/05/23 | 00:30 | America FC MG vs Fortaleza EC CE | 2.45 | 3.40 | 2.60 |
| 09. 21/05/23 | 14:30 | Club Brugge vs Royal Antwerp FC | 2.23 | 3.20 | 2.65 |
| 10. 21/05/23 | 15:30 | SK Rapid Wien vs LASK | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 21/05/23 | 15:30 | West Ham United vs Leeds United | 2.22 | 3.35 | 2.95 |
| 12. 21/05/23 | 16:30 | FSV Mainz vs VfB Stuttgart | 2.35 | 3.40 | 2.70 |
| 13. 21/05/23 | 19:00 | SSC Napoli vs Inter Milano | 2.90 | 3.25 | 2.28 |
| 14. 21/05/23 | 19:00 | Adana Demirspor vs Besiktas Istanbul | 2.48 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 21/05/23 | 19:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.17 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 21/05/23 | 21:30 | CA Belgrano vs CA Talleres de Cordoba | 2.95 | 2.85 | 2.22 |
| 17. 21/05/23 | 22:30 | Sporting Lisbon vs Benfica Lisbon | 2.48 | 3.45 | 2.50 |

MECHI ZA USHINDI
“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE
“2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 19/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:45 | 5297 | Melbourne City vs Sydney FC | 1.87 | 3.58 | 3.68 |
| 13:30 | 1612 | Consadole Sapporo vs Kyoto Sanga | 1.63 | 3.89 | 4.20 |
| 14:00 | 3635 | SC Dnipro 1 vs Kolos Kovalivka | 1.31 | 4.60 | 7.77 |
| 14:35 | 2816 | Shanghai Shenhua vs Beijing Guoan | 2.27 | 2.98 | 2.98 |
| 17:00 | 2665 | Shakhtar Donetsk vs Veres Rivne | 1.17 | 5.96 | 11.30 |
| 17:00 | 5272 | Slaven Belupo vs Hajduk Split | 3.69 | 3.38 | 1.84 |
| 17:45 | 3818 | AL Qadsia vs Kazma SC | 2.24 | 3.15 | 2.70 |
| 19:05 | 2969 | HNK Sibenik vs NK Osijek | 2.83 | 3.14 | 2.28 |
| 19:15 | 2741 | Paksi FC vs Puskas Akademia | 2.07 | 3.46 | 3.05 |
| 19:30 | 2494 | SV Darmstadt vs Magdeburg | 1.44 | 4.77 | 5.68 |
| 19:30 | 3565 | Holstein Kiel vs St. Pauli | 2.88 | 3.69 | 2.16 |
| 20:00 | 1230 | IK Brage vs Gefle IF | 1.71 | 3.80 | 4.49 |
| 20:00 | 5914 | Grenoble Foot vs Rodez Aveyron | 2.44 | 3.15 | 2.75 |
| 20:30 | 3904 | Josko Ried vs SCR Altach | 2.05 | 3.29 | 3.14 |
| 21:00 | 1236 | Jong AZ Alkmaar vs ADO Den Haag | 2.25 | 3.58 | 2.70 |
| 21:00 | 1796 | Jong Utrecht vs VVV Venlo | 3.13 | 3.55 | 2.02 |
| 21:00 | 1892 | Dordrecht vs FC Oss | 2.05 | 3.49 | 3.12 |
| 21:00 | 2198 | Jong PSV vs FC Eindhoven | 2.65 | 3.38 | 2.37 |
| 21:00 | 2628 | Helmond Sport vs PEC Zwolle | 5.64 | 4.91 | 1.40 |
| 21:00 | 2756 | Almere City vs Maastricht | 1.51 | 4.37 | 4.90 |
| 21:00 | 3523 | Heracles Almelo vs Jong Ajax | 1.32 | 5.59 | 6.42 |
| 21:00 | 5897 | Dhamk vs Al Hilal Riyadh | 4.99 | 3.93 | 1.63 |
| 21:15 | 5432 | FC Aarau vs FC Schaffhausen | 1.54 | 3.95 | 4.82 |
| 21:15 | 5881 | FC Thun vs Lausanne-Sport | 2.15 | 3.38 | 2.87 |
| 21:30 | 1155 | SC Freiburg vs VfL Wolfsburg | 2.26 | 3.45 | 2.80 |
| 21:30 | 1393 | Genoa vs Bari | 1.75 | 3.51 | 4.29 |
| 21:30 | 1477 | Perugia vs Benevento | 1.73 | 3.46 | 4.50 |
| 21:30 | 2087 | Ternana vs Frosinone | 3.34 | 3.34 | 2.04 |
| 21:30 | 2558 | Kisvarda FC vs Vasas SC | 1.72 | 3.54 | 4.26 |
| 21:30 | 2642 | Modena vs Sudtirol | 2.60 | 3.03 | 2.66 |
| 21:30 | 2673 | Pisa vs Spal | 1.63 | 3.66 | 4.91 |
| 21:30 | 2691 | Cosenza vs Cagliari | 3.18 | 3.34 | 2.10 |
| 21:30 | 3795 | Reggina vs Ascoli | 2.11 | 3.20 | 3.30 |
| 21:30 | 4070 | Palermo vs Brescia | 1.97 | 3.36 | 3.51 |
| 21:30 | 4640 | Cittadella vs Como | 2.00 | 3.24 | 3.56 |
| 21:30 | 5073 | Korona Kielce vs Lech Poznan | 3.99 | 3.64 | 1.71 |
| 21:30 | 5439 | Parma vs Venezia | 2.23 | 3.09 | 3.14 |
| 21:45 | 2778 | Shelbourne vs St Patricks | 2.46 | 3.12 | 2.61 |
| 21:45 | 3100 | Derry City vs UCD Dublin | 1.13 | 6.15 | 16.41 |
| 21:45 | 3476 | Sassuolo vs Monza | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 21:45 | 4730 | Dundalk FC vs Bohemians FC | 2.48 | 3.08 | 2.62 |
| 21:45 | 5593 | Partick Thisle vs Ayr United | 1.88 | 3.52 | 3.73 |
| 21:45 | 5906 | Cork City vs Sligo Rovers | 3.12 | 3.27 | 2.07 |
| 22:00 | 1361 | Barnsley vs Bolton | 1.97 | 3.43 | 3.58 |
| 22:00 | 2752 | Al Ahly Cairo vs Esperance Tunis | 1.86 | 2.95 | 4.32 |
| 22:00 | 3070 | Shamrock Rovers vs Drogheda Utd | 1.31 | 4.52 | 7.81 |
| 22:00 | 4133 | Cadiz CF vs Valladolid | 2.16 | 3.24 | 3.14 |
| 22:00 | 4466 | Lyon vs Monaco | 2.18 | 3.75 | 2.75 |
| 22:15 | 2806 | Maritimo vs FC Vizela | 1.81 | 3.66 | 3.87 |
| 22:30 | 5208 | CD Palestino vs O Higgins | 2.04 | 3.36 | 3.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Mei 19, 2023
Nipashe

**Rashford arejea mazoezini United**
UKURASA 22






# RAIS SAMIA AIPA NDEGE YANGA SC

## ●●●Aahidi kutoa Sh. milioni 20 wakishinda, pongezi zamiminika...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ameipongeza Yanga kwa kutinga fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, kiongozi huyo mkuu pia ametoa ndege kwa ajili ya kuipeleka timu hiyo Algeria katika mechi ya marudiano dhidi ya wenyeji, USMA Alger itakayochezwa Juni 3, mwaka huu.

Yanga itacheza mechi yake ya kwanza ya hatua ya fainali Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Rais Samia alisema jana ndege hiyo itawasubiri wachezaji, viongozi na baadhi ya mashabiki wa Yanga watakaosafiri katika mechi hiyo ya mkondo wa pili na amewataka ushindi.

Pia kiongozi huyo namba moja Tanzania ameahidi kutoa Sh. milioni 20 kama itafanikiwa kushinda mechi ambayo itaipa timu hiyo ushindi.

"Sasa Yanga inakwenda kwenye fainali, tunapokwenda fainali ni Sh. milioni 20 kama timu ikitoka na ushindi, hii haitakwenda kufungwa mbili, kufunga moja hapana, yawe magoli yote yameipa timu hii ushindi, kila goli milioni 20, lakini zaidi ya hapo, serikali itatoa ndege kuwapeleka katika mchezo wa fainali," alisema Rais Samia jijini jana.

Aliongeza hatua ambayo Yanga imefika ni kubwa na imeiletea nchi heshima.

"Pongezi za dhati kwa klabu ya Yanga kwa kutinga fainali ya Kombe la Shirikisho (CAF Confederation Cup). Mmeandika historia na kuipa nchi yetu heshima kubwa sana. Nawatakia kila la kheri katika mchezo wenu wa fainali," aliandika rais huyo.

Naye Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, ameipongeza Yanga kwa kutinga fainali, ikiwa ni kwa mara ya pili nchi ikiingia hatua hiyo baada ya miaka 30.

Karia alisema anatamani kuona kiongozi wa Algeria naye akabidhi kombe la ubingwa kwa wageni kama Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, alivyowakabidhi Stella Abidjan ya Ivory Coast iliposhinda dhidi ya Simba, katika mechi ya fainali iliyochezwa Tanzania.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza Yanga, naamini mwaka huu, sisi tutacheza hapa tutawafunga, tutakwenda kwao, kiongozi wa Algeria atawapa kombe Yanga, kama ambavyo lilichukuliwa hapa, na sisi tutalichukua kwao," alisema Karia.

Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo' aliandika kwenye mtandao wake wa 'Twitter' kuipongeza Yanga kwa mafanikio waliyopata.

"Hongera sana mtani, umefanya Tanzania ijivunie." Aliandika Dewji.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wamefanya kazi kubwa na wamestahili kufika hapo na sasa wanapaswa kumalizia pale walipoishia.

INAENDELEA UK. 23

## Simba yatangaza dk. 180 za furaha

**Na Saada Akida**

BAADA ya mapumziko ya siku nne kumalizika, kikosi cha Simba kimerejea mazoezini ili kujiandaa na mechi mbili zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania na Coastal, lakini pia maandalizi ya msimu mpya.


Mazoezi hayo yamefanyika kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju Dar es Salaam chini ya Kocha Mkuu, Robert Oliveira 'Robertinho' ambaye alisema wachezaji wote wameshiriki programu hiyo.

Robertinho alisema anaimani mchezo ujao watavuna pointi tatu ili kumaliza ligi kwa heshima.

"Tunajiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kwa kuvuna pointi sita ili kumaliza ligi kwa heshima na kuanza kujiandaa kwa msimu mpya," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaimani na wachezaji

INAENDELEA UK. 23



## Guardiola atamba sasa ni zamu yao

UKURASA. 21

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >